


UKURASA 4



**DK. MWINYI** ajibu hoja nyeti zilizoibuliwa na ACT-Wazalendo


UVCCM yaanza mwaka kwa kishindo, yaanzisha mpango wa kurejea darasani

Ukurasa 12

Ukurasa 14

siasa

JUMATANO MACHI 1, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

SHAMIM KHAN Mbunge, waziri aliyeacha nyayo kuinua wanawake kwenye uchumi na biashara

WANAHABARI WATAKA SMZ IWAPE RAHA

Ni kuwaondolea Sheria ya Usajili wa Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu

■ Inaongeza hofu, kuwapa polisi kazi za 'kubinya media'

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

UKURASA 11

Jumatano Machi 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581236

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


LIKE & FOLLOW US

# 'ACHENI HOFU'

**NAPE** awataka wanahabari kumsaidia Rais kufichua madudu' ... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea hati ya utambulisho kutoka kwa Balozi wa Jamhuri ya Slovak hapa nchini, Katarina Zuffa Leligdonova, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye

# Lema kutua nchini bila mke, watoto

UKURASA 2



Godbless Lema

# Kanisa Kuu lililovunjwa altare sasa lafungwa

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA YASHUSHA PONGEZI SIMBA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

# Nape awataka wanahabari kuacha hofu

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amewataka waandishi wa habari kuwa jicho la Rais Samia Suluhu Hassan ili kusaidia kufichua madudu yaliyoko ndani ya taasisi za serikali na kufanya ukosoaji wenye kujenga badala ya kukomoa.

Sambamba na hayo, amewataka wanahabari kuandika kwa uhuru bila woga habari ambazo zitajenga taswira ya nchi.

Nape aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam baada ya kufanya ziara ya kutembelea vyombo vya habari vya IPP na kushuhudia namna vinavyofanya kazi.

Alisema katika salamu zake, Rais amewaomba waandishi wa habari kushiriki kwa kuwa jicho lake lingine, kusaidia kufichua kasoro na changamoto zilizopo kwa sababu anajua hawezi kuwa kila mahali.

"Mkitusaidia kufichua mapungufu (upungufu) yaliyopo (uliopo). Tunajua si lugha iliyozoeleka. Ukificha maradhi mauti itakukuta. Tungetamani tuyaseme maradhi kwamba kuna mkono unauma mahali tuseme, kuna jicho linauma mahali tuseme.

"Tofauti kubwa ambayo inakuwapo ni staha ya usemaji kwamba ninyi (IPP) mmekuwa vizuri mnafanya vizuri sana tunaona taarifa zenu namna mnavyozipeleka unaona hawa wana lengo. Kuna kukosoa kwa lengo la kutibu kuna kukosoa kwa lengo la kukomoa, ni vitu viwili tofauti," alisema.

Nape alivieleza vyombo vya habari vya IPP kuwa amefika hapo kuwathibitishia kwamba serikali inawaunga mkono na kuomba waendelee kutoa taarifa na kusaidia.

"Nchi ni ya kwetu sote kwa pamoja tukishikamana pamoja inawezekana, tuondoe ubaridi, tuondoe hofu, zama za hofu zimekwisha," alisema.

"Tunatamani kuona ile mijadala ya moto, twendeni huko ni rahisi kukumbuka viboko, basi usikumbuke viboko kumbuka hii nia njema ya serikali ya kutaka twende huo," alisisitiza.

Waziri huyo alitumia fursa hiyo kuvipongeza vyombo vya habari vya IPP kwa kufanya kazi vizuri na kueleza kuwa sio kati ya vyombo wanavyokimbizana navyo.

"Kesi nyingi hatuzisikii, toka nimeingia sijasikia kesi kutoka kwenu. Pia tumejitahidi sisi wenyewe vyombo vinavyosimamia sekta ya habari viwe wazazi zaidi kuliko kuwa polisi na kuchapana viboko. Tunaweza kuambiana, kushauriana lengo letu wote ni kujenga," alisema.



Aidha, aliviomba vyombo vya habari kushiriki kutoa maoni kwenye muswada wa marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 iliyopelekwa bungeni.

Pia alitaka washiriki kutoa maoni yao kupitia kamati ya kuangalia hali ya uchumi wa vyombo vya habari, ili serikali ione namna bora ya kusaidia kupunguza madhara yanayotokana na msukosuko tuliopitia baada ya UVIKO -19 na vita vya Ukraine.

"Uchumi wa vyombo vya habari umeyumba na gharama za uendeshaji kukua kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19 na vita vya Ukraine, wenzenu wa magazeti wameteseka zaidi, Rais ametuagiza tuangalie namna ya kushughulika nalo.

"Serikali imeshughulika na sekta nyingine kama ya utalii zilitafutwa fedha za kufidia madhara, elimu kuna madarasa kwa sasa yanaitwa UVIKO-19 na kwenye afya pia.

"Kwenye tasnia ya habari nao wameathirika lakini hatujaona namna bora ya kusaidia kupunguza madhara yanayotokana na msukosuko tuliopitia, tukafikiri serikali isije na suluhisho yenyewe, tukaunda timu na Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile ni mjumbe," alisisitiza.

Alisema wanaamini timu hiyo itakuja na mawazo ya namna bora ya kusaidia uchumi wa vyombo vya habari.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
01.03.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 03-03-2023** kampuni ya **Spedag Interfreight Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es- Salaam Port** kuelekea **Mzenga**, gari hiyo ina namba ya usajili: **DS00TGP / NRB 23609**
2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 35.50**
   **Upana - mita 7.50**
   **Kimo - mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: Bandari ya **Dar-Es-Salaam hadi Mzenga kupitia Morogoro Road** Gari itasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka Dar- Es- Salaam Port mpaka Mlandizi Kutoka **Mlandizi kwenda Mzenga** gari itasafiri muda wa mchana ***(kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## Lema kutua bila mke na watoto

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kanda ya Kaskazini kimesema kimekamilisha utaratibu wa kumpokea Mjumbe wa Kamati Kuu na aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless lema.

Aidha, kimesema atapokelewa na viongozi wa CHADEMA Taifa na baadaye atapumzika kwa wiki mbili kwa ajili ya masuala ya kifamilia. Lema anatarajiwa kuingia nchini huku mke na watoto wakiwa bado uhamishoni.

Lema anatarajiwa kuwasili nchini leo majira saa 6:30 mchana kwa Ndege ya Shirika la Ethiopia kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) baada ya kukaa nje ya nchini kwa miaka miwili.

Kiongozi huyo alikuwa Mbunge wa Arusha Mjini kwa miaka 10 mfululizo kuanzia 2010. Aliondoka na familia yake na kwenda nchini Kenya Novemba 8, 2020 ambako alikaa kwa mwezi mmoja, kabla ya kuondoka nchini humo Desemba 8, mwaka huo huo kwenda Canada, alikopata hifadhi ya kisiasa kwa madai ya kuwapo kwa tishio la kuuawa yeye na familia yake.

Mwanasiasa huyo kijana, aliyekuwa mkosoaji mkubwa wa serikali ya Hayati Rais Dk. John Magufuli, anakuwa kiongozi wa pili wa CHADEMA kurejea nchini akitokea uhamishoni, baada ya Januari 25, mwaka huu, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, naye kurejea akitokea uhamishoni Ubelgiji.

Akizungumzia mapokezi ya Lema, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Amani Golugwa, alisema chama kimeandaa mapokezi makubwa ya kiongozi huyo, ambaye ni mwenyekiti wa chama hicho, Kanda ya Kaskazini.

"Mheshimiwa Lema atapokewa na viongozi wengi akiwamo Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe. Watakuwapo wajumbe wengine wa kamati kuu, viongozi mbalimbali kutoka mikoa yote kutoka kanda 10 za Tanganyika na Zanzibar.

"Atakuwapo pia mwanasheria wake, aliyekuwa mgombea urais nchini Kenya, Prof. George Wajakoya, wanachama na wakazi wa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

"Unajua Lema amekuwa Mbunge wa Arusha kwa kipindi cha miaka 10, kwa hiyo tunatarajia atapata mapokezi ya makubwa na atakapopokewa, atakuwa na msafara mrefu sana kutoka KIA kwenda Arusha kwenye mkutano wa hadhara utakaofanyika uwanja wa relini siku hiyo hiyo (leo). Mkutano huo unatarajiwa kuanza majira ya alasiri," alisema.

Alipoulizwa kama Lema anarejea nchini na familia yake, Golugwa alisema: "Hapana! haji na familia yake. Mke wake (Anna Tarimo) na watoto wake watatu kwa kipindi hiki hawatakuja. Kwa hiyo atakuwa mwenyewe."

"Pale uwanjani atapokewa na wazazi wake, baba yake na mama yake lakini pia na wadogo zake. Atatumia barabara ya Mianzini kupitia barabara ya Maji kwenda moja kwa moja uwanja wa Relini."

**MAPUMZIKO WIKI MBILI**

Kuhusu ushiriki wake katika uzinduzi wa mikutano mikoani, Katibu huyo wa Kanda alisema kwa kuwa Lema ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, atakuwa na kazi nyingi za Kanda ya Kaskazini.

"Mheshimiwa Lema hakuwapo nchini kwa takribani miaka miwili sasa. Kwa hivyo tulishauriana naye kama chama, na tukampa wiki mbili za kupumzika na kwenda nyumbani (Machame) kukaa na familia.

"Baada ya hapo, atakuwa na vikao vya kiutendaji ngazi ya kanda, atashiriki siku ya wanawake duniani Machi 8 mwaka huu, ambayo kichama na kitaifa inafanyika Mkoa wa Kilimanjaro.

"Baadaye atashiriki ziara ambazo tumezipanga za mikutano ya hadhara kwenye kanda. Ataweka nguvu kubwa kwanza kwenye kanda ya kaskazini kama tulivyopanga ratiba, na baadaye tutamruhusu angalau kwenda kwenye mikutano ya ziara za kitaifa," alisema.

"Lakini tumempa kazi kubwa zaidi ya kufanya kwenye mikoa ya kanda ya kaskazini na hasa Jimbo la Arusha, kwanza! Atafanya kazi hiyo ya mikutano ya hadhara kwenye kata 25 za Jimbo la Arusha na baadaye kwenye kanda nzima," aliongeza.

**PROF. WAJACKOYAH AFUNGUKA**

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mapokezi hayo, Mwanasheria wa Lema, Prof. Wajackoyah, alisema Lema ana ukomavu wa kisiasa.

"Nilipambana kumsaidia Godbless Lema kutokana na maisha yake kuwa hatarini kisiasa na nikafanikisha kuwasiliana na mashirika mbalimbali ya haki za binadamu hasa Amnesty International (Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Binadamu) na mengineyo ili kuhakikisha Lema anapata hifadhi.

"Nia yangu ilikuwa ni kumtoa mikononi mwa Polisi wa Kenya, waliotaka kumrejesha nchini Tanzania," alibainisha.

Alisema alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu kuruhusu mikutano ya siasa na kuita kuwa hiyo ndio demokrasia ya kweli.

Kwa mujibu wa Wajackoya, amekuja kushuhudia ujio wa Lema ambaye amekuwa Canada kwa zaidi ya miaka miwili sasa na kwamba alifurahishwa na uamuzi wa kuruhusiwa kwa mikutano ya hadhara nchini.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Hussein Mwinyi (katikati), akishuhudia utiaji saini wa mkataba wenye thamani ya Euro milioni 540 sawa na (Sh. trilioni 1.3) kati ya Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na benki tatu za Tanzania ikiwamo KCB Tanzania wenye lengo la kusaidia wanawake wanaongoza biashara na sekta ya uchumi wa bluu, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Makamu wa Rais wa EIB, Thomas Ostros, Mkurugenzi wa Kamisheni ya Fedha, Uwekezaji na Ajira, Antii Kurhunen na (kulia) ni Kaimu Mkurugenzi wa Biashara wa Kanda wa KCB Group na Mkurugenzi Mtendaji wa KCB Bank Tanzania, Cosmas Kimario na wakuu wa benki nyingine. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Kanisa lililovunjwa altare lafungwa

**Na Mwandishi Wetu**

KANISA Kuu la Kiaskofu la Jimbo Katoliki la Geita, limefungwa kwa muda maalum kutoa huduma zote za kiibada kuanzia Februari 27 hadi Machi 18, mwaka huu, kupisha ukarabati na kuweka upya wakfu wa nyumba hiyo ya ibada.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Geita, Flavian Kassala, kuanzia juzi kanisa hilo halitatoa huduma za kiibada na kisakramenti kutokana na tukio la kufuru kubwa ya sakramenti takatifu na unajisi utakatifu wa jengo uliofanyika ndani ya kanisa.

"Kwa dikrii hii, mimi Flavian Kassala, ambaye kwa neema ya Mungu na mamlaka ya kiti cha kitume na Askofu wa Jimbo Katoliki la Geita na kwa mamlaka niliyopewa na Sheria Kanuni ya Kanisa na kwa maelekezo ya Mamlaka ya Kiaskofu natamka kuwa uharibifu uliofanyika Februari 26, mwaka huu, umeivunjia sakramenti ya ekaristi takatifu heshima yake kwa kiasi kikubwa," alisema.

Alisema tukio hilo ni kufuru kubwa kwa sakramenti na limelinajisi kanisa katika utakatifu wake uliowekwa wakati wa kutabarikiwa na kwamba umeiathiri kwa kiasi kikubwa hadhi na muumini Mkatoliki na jamii yetu kwa ujumla.

"Kutokana na matukio hayo, kanisa hili limepoteza kwa kiasi kikubwa baraka yake na jamii ya waamini imeumizwa sana kutokana na kashfa, kufuru na unajisi uliofanyika kwa imani yetu. Na hivyo ninaagiza kwamba: Kanisa Kuu la Kiaskofu la Jimbo Katoliki la Geita halistahili kwa maadhimisho ya Sakramenti ya Ekaristi, wala ya Sakramenti yoyote, wala kwa ibada yoyote.

"Kufuatia hali hii, Kanisa Kuu la Kiaskofu la Geita litabaki limefungwa kwa huduma zote za kiibada kuanzia Februari, 2023 hadi Machi 18, 2023, ili kusubiri Utakaso wake," alisema.

Askofu Kassala alisema kwa kipindi hicho cha kufungwa kwa Kanisa, familia nzima ya Mungu Jimboni Geita inaingia katika kipindi cha siku 20 za kuelekea adhimisho la toba ya malipizi kwa siku zote linapofungwa.

Aidha, alisema kwa kipindi chote cha kuelekea toba mapadre waandae na kuwaandaa waamini katika Jimbo kwa ibada za upatanisho, mahubiri ya toba, na mafundisho juu ya utakatifu wa kanisa na kuyatoa daima kwa waamini wao ndani ya maadhimisho mbalimbali.

"Kwa kipindi chote cha kuelekea toba ya malipizi waamini wote wakatoliki wanaalikwa kusali, kufunga, kutubu, kupokea sakramenti ya upatanisho na kuomba huruma ya Mungu. Katika matendo yote haya tuombe Mungu atujalie wongofu wa ndani," alisema.

Alisema kanisa hilo litafunguliwa machi 18, kwa ibada ya Misa Takatifu kuanzia saa 4:00 asubuhi itakayohusu pia maadhimisho ya toba ya malipizi, baraka, kutakatifuza kanisa kuu na kurudisha ekaristi takatifu ndani ya kanisa na kwamba wote wenye mapenzi mema wanaalikwa kushiriki.

Wakati huo huo, Askofu Mkuu wa Jimbo la Dar es Salaam, Yada Thadeus Ruwai'chi, alisema kitendo hicho ni makwazo kwa kanisa na kwamba sio matendo yanayopaswa kushabikiwa, kuvumiliwa au kuigwa na yeyote.

"Kushabikia, kuiga au kutekeleza vitendo vya kufuru kama vilivyofanyika ni sawa na kujilaani mwenyewe, kilichofanyika ni kunajisi kanisa, ninatoa pole kwa Askofu, Mapadri, watawa na waumini wa Geita, tupo pamoja nanyi kuwaombea baraka za Mungu mnapokabili mambo haya magumu," alisema. "Naomba nitoe onyo, kulingana na imani zetu kanisa ni mahali wakfu, ni mahali palipowekwa rasmi kwa ajili ya Mungu, kwa ajili ya maadhimisho matakatifu na kwa ajili ya utakatifuzo wa watu, sio mahali ambako mtu anaweza kwenda na kufanya vurumai zake atakavyo," alifafanua.

Kwa mujibu wa Askofu Ruwai'chi, kanisa linapopatwa na jambo kama hilo kinachopaswa kufanyika, ili huduma ziendelee ni "Kwa kaiwada kanisa likinajisiwa kama hilo lilivyofanyiwa, litahitaji kufanyiwa ukarabati, yaliyoharibiwa yarudishwe yawekwe sawa na baadaye liwekwe wakfu upya."

"Naamini waumini wetu wa Geita watajikusanya na kukarabati yaliyovurugwa na kuharibiwa na baadaye kanisa litawekwa wakfu upya,"alisema.


MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA

## TAARIFA KWA UMMA

### Kuondolewa kwa Ukomo wa Matumizi ya Vitambulisho vya Taifa

***Dar es Salaam; Machi 01, 2023***

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inapenda kuwafahamisha wananchi wote wenye Vitambulisho vya Taifa ambavyo vina tarehe ya ukomo wa matumizi kwa mujibu wa Kanuni ya 7 (2) (v) ya Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za Mwaka 2014 kwamba, Serikali kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, imeondoa ukomo wa matumizi ya Vitambulisho kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN) Na. 96 la tarehe 17 Februari, 2023.

Hivyo basi, watoa huduma wote nchini wanaotumia Vitambulisho vya Taifa katika kuwahudumia wananchi wazingatie maelekezo ya Serikali ya kuendelea kuvitambua na kuvitumia Vitambulisho vya Taifa ambavyo vina tarehe ya muda wa ukomo uliopita kwa kuwa Vitambulisho hivyo havitakuwa na ukomo wa matumizi.

Marekebisho haya hayahusishi Vitambulisho vya Wageni Wakaazi na Wakimbizi na hivyo muda wa Vitambulisho hivyo uzingatiwe pale vinapotakiwa kuhuishwa.

Imetolewa na;

**Kitengo cha Mawasiliano na Hifadhi Hati,**
**Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)**

# Mwinyi ajibu hoja zilizoibuliwa na ACT

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema hoja zote zilizotolewa na viongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo mwishoni mwa wiki katika mkutano wa hadhara wa chama hicho dhidi ya serikali ni za upotoshaji na hazina nia ya kujenga nchi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari Ikulu, Zanzibar ukiwa ni utaratibu wake wa kukutana na waandishi wa habari kila mwisho wa mwezi.

Dk. Mwinyi alisema demokrasia inahitaji mambo ya kujenga na si kuzusha mambo yasiyo na uhalisia ili kuwapotosha wananchi.

"Nashurukku mikutano ya hadhara imeanza na ni jambo la kidemokrasia na nashukuru mikutano imefanyika kwa amani na utulivu lakini ni bahati mbaya tu wazungumzaji sijawajisikia wakihimiza amani, utulivu, mshikamano na maridhiano. Sisi Chama Cha Mapinduzi tutaendelea kuwa hiyo ni ajenda yetu namba moja," alisema.

Akijibu hoja za ACT-Wazalendo kuhusu Bandari ya Malindi, alisema hakuna asiyejua kuwa bandari hiyo ina changamoto na sababu kuu ya kuwa na gati moja na kusababisha ucheleweshaji wa ushushaji wa meli za mizigo.

Meli ya mizigo, alisema huchukua wastani wa siku saba kwa meli moja kushusha mzigo, hivyo kuna uhitaji wa bandari kubwa na ndio mipango ya serikali yake.

Alisema ujenzi wa bandari ya Mangapwani utasaidia kuondoa tatizo hilo na chama hicho kuendelea kulaumu kwa jambo ambalo lipo muda mrefu kabla ya utawala wake si jambo sahihi.

Dk. Mwinyi alisema serikali yake imechukua hatua na kuingiza zana mpya katika bandari hiyo lengo ni kuongeza kasi ya upakiaji na ushushaji wa mizigo bandarini hapo.

Alisema si kwamba hatambui changamoto zilizoko bandarini, hivyo ni vyema ACT ikashauri kuliko kulaumu kwa sababu wanaongoza serikali pamoja katika mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kwamba lawama walizozitoa hazina uhalisia bali zina lengo la kupotosha umma.

Kuhusu kampuni ya Dnata kutoka Dubai inayotoa huduma katika jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Dk. Mwinyi alisema serikali imeamua kutoa tenda kwa kampuni hiyo kwa sababu kampuni za wazawa zilizokuwapo zimekaa zaidi ya miaka 25 na serikali haikuwa ikipata faida.

Alisema wakati serikali ya awamu ya nane inaingia madarakani ilikuwa ikipata hasara na hulazimika kutoa fedha kutoka hazina kupeleka mamlaka ya viwanja vya ndege kwa ajili ya kulipa mishahara ya wafanyakazi.

"Katika maegesho ya magari katika viwanja hivyo kampuni imekusanya Sh. milioni 139 kwa mwezi mmoja uliopita wakati kampuni ya wazawa iliyokuwa ikisimamia maegesho hayo ilikuwa ikipata Sh. milioni mbili.

"Haya mbona hawayasemi? Hao wanaowataka wao wana maslahi gani? Upo uhusiano kati ya hizo kampuni za wazawa na viongozi mbona hawasemi? Kwa hiyo hapa hawatetei serikali na nchi wanatetea maslahi binafsi kwa sababu hizo kampuni zinalipa asilimia tano serikalini lakini Dnata inalipa asilimia 32 nani anayetetea maslahi ya umma," alisema.

Akijibu tuhuma kuhusu miradi ya wajasiriamali iliyotokana na fedha za ahueni za UVIKO-19 kwamba vikundi vilivyopatiwa fedha hizo ni kutoka CCM na Sh. bilioni 31 zimetumika vibaya hakuna ukweli katika hilo.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akizungumza na uongozi mkuu wa Bolt kimataifa uliomtembelea ofisini kwake, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine (kutoka kushoto) ni Meneja Mwandamizi wa Sera za Umma Afrika Mashariki na Kusini, Andrew Ihsaan, Mkuu Mwandamizi wa Sera ya Umma Afrika, Kenneth Anye na Makamu wa Rais Sera na Udhibiti, Eirini Zafeiratou. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ndugu aliyegongwa ajali mwendokasi wajitokeza, wamtambua na kutoa neno

**Na Mary Geofrey**

SIKU tano baada ya basi la mwendokasi kupata ajali eneo la Kisutu, Dar es Salaam na kumgonga mtembea kwa miguu, Osam Milanzi, ndugu zake wamejitokeza na kumtambua wakati hali yake ikiendelea kuimarika.

Milanzi ambaye alihesabika kama mtu asiyejulika, alilazwa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), akiendelea na matibabu baada ya kujeruhiwa vibaya.

MOI ilitangaza kutafuta ndugu wa Milanzi hadi hapo walipojitokeza juzi na kumtambua mgonjwa wao ambaye awali alilazwa chumba cha wagonjwa walio katika uangalizi maalum (ICU).

Taarifa iliyotolewa jana na Meneja Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, ilieleza kuwa ndugu waliojitokeza ni mke wake, Isha Mohamed na mdogo wake, Shaban Milanzi.

Alisema Milanzi ni mkazi wa Manzese Midizini, Dar es Salaam na alilazwa hospitalini hapo baada ya kupata ajali iliyojeruhi zaidi ya watu 30 ambao wengine wote walitambuliwa na ndugu na kuruhusiwa baada ya afya zao kuimarika.

Mvungi alisema Milanzi alikuwa kama mgonjwa asiyetambulika (unknown) na juzi ndugu zake walijitokeza kumtambua na kumkuta afya yake ikiwa tayari imeimarika tofauti na alivyofikishwa hospitalini hapo.

"Afya ya ndugu Milanzi imeimarika sana kutokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na madaktari, wauguzi na watumishi wengine wa MOI," alisema Mvungi.

Akizungumza jana, mke wa Milanzi alisema hakupata taarifa kwa wakati kwa sababu siku anaenda kazini Jumatano, alifikiri amesafiri kwa sababu aliaga angesafiri kwenda kwenye shughuli zake za uvuvi.

"Jana (juzi) nilipata taarifa kwa shemeji yangu baada ya kunionyesha 'clip' ambayo nilivyoiona nilimbaini kwa asilimia 90 ni mume wangu kupitia shati alilovaa siku anaondoka," alisema Isha.

Alieleza kuwa, walitoka nyumbani juzi kuelekea MOI ambako walimkuta mgonjwa akiwa anaendelea vizuri.

"Kwa jinsi nilivyoona 'clip' hali aliyokuwa nayo kutokana na ajali ile, nimemkuta anaongea, amenifahamu, Namshukuru Mungu sana, kiukweli niishukuru MOI kwa kupambania afya yake na mitandao ya kijamii," alisema Isha.

Naye mdogo wa Milanzi, alisema hali ya mgonjwa ni nzuri kulinganisha na namna alivyopata ajali hawakutarajia kama wangemkuta na hali hiyo.

"Tunawashukuru wasamaria wema, madaktari wanavyopambania afya yake kama ndugu yao na hali tuliyomkuta nayo Mungu awabariki sana. Tumefurahi kumwona ndugu yetu akiwa hai," alisema Shaban.

Jumatano iliyopita, basi la mwendokasi liligongwa na gari dogo eneo la Kisutu, wakati likitokea Posta na kumgonga mtembea kwa miguu Milanzi, ambaye alitambulika kupitia video fupi ya CCT-Camera iliyokuwa ikisambaa kwenye mitandao ya kijamii.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

TAARIFA KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SUMBAWANGA

Mnamo tarehe 30 Disemba 2022 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za huduma za maji safi na usafi wa mazingira kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga. Majedwali Namba 1 hadi 5 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga.

Jedwali Na. 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa

| Kundi la Wateja | Matumizi($m^3$) | Kipimo | Bei ya Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 0-5 | Sh./$m^3$ | 1,000 | 1,603 | 1,768 | 1,854 |
| | Zaidi ya 5 | | 1,245 | 1,995 | 2,201 | 2,308 |
| Taasisi | | | 1,280 | 2,052 | 2,263 | 2,373 |
| Biashara | | | 1,280 | 2,052 | 2,263 | 2,373 |
| Viwanda | | | 1,480 | 2,372 | 2,617 | 2,743 |
| Magati | | Sh./L.20 | 20 | 30 | 40 | 50 |

Jedwali Na. 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shlingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 15,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Biashara | 15,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Viwanda | 15,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |

Jedwali Na. 3: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani<br>Taasisi<br>Biashara<br>Viwanda | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | Kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na.5 ya Mwaka 2019 | | |

Jedwali Na.4: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Uondoaji wa Majitaka (Shilingi kwa Tripu)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2021/22 |
| Majumbani | 80,000 | 90,000 | 100,000 | 120,000 |
| Taasisi | 90,000 | 120,000 | 130,000 | 150,000 |
| Biashara | 120,000 | 120,000 | 130,000 | 150,000 |
| Viwanda | 150,000 | 150,000 | 160,000 | 170,000 |

Jedwali Na. 5: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kumwaga Majitaka kwenye Mabwawa ya Sumbawanga WSSA (Shilingi kwa Tripu)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2021/22 |
| Majumbani | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 25,000 |
| Taasisi | 25,000 | 25,000 | 25,000 | 35,000 |
| Biashara | 35,000 | 35,000 | 35,000 | 50,000 |

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Sumbawanga WSSA ilieleza kuwa bei, ada, na tozo zinazopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kukidhi ongekezo la gharama za uendeshaji na uwekezaji ili kutoa huduma bora na endelevu kwa wakazi wa mji wa Sumbawanga.

Tangazo hili limetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA Sura ya 414, kinachoitaka EWURA kutoa tangazo la taftishi ili kukusanya maoni kutoka kwa wadai ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali (EWURA GCC), Baraza Ushauri la Watumiaji wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC), Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga na Umma kwa ujumla kuhusu bei zinazopendekezwa. Kama sehemu ya taftishi, kutakuwa na mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau utakaofanyika siku ya Alhamisi, tarehe 9 Machi 2023 katika Ukumbi wa Libori uliopo katika Manispaa ya Sumbawanga kuanzia saa nne asubuhi.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo juu wakati wowote hadi tarehe 15 Machi 2023. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga yanaweza kupatikana kwenye ofisi za Makao Makuu ya EWURA zinazopatika katika Jengo la EWURA, Medeli Magharibi, Dodoma au Ofisi za EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zilizopo Ghorofa ya Sita, Jengo la NHIF, Mtaa wa Karume, Mbeya Mjini au kwenye ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga.

**Mkurugenzi Mkuu**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S. L. P 2857, Dodoma.
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005; Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mawaziri wazingatie kauli ya Rais kuhusu utendaji kazi wao

**RAIS** Samia Suluhu Hassan juzi aliwaapisha viongozi wapya aliowateua na wengine aliowabadilisha nafasi za uongozi katika sherehe zilizofanyika Ikulu, Chamwino jijini Dodoma.

Tangu aingie madarakani takriban miaka miwili iliyopita, Rais Samia amefanya mabadiliko makubwa manne katika Baraza la Mawaziri pamoja na kufanya uteuzi wa ngazi mbalimbali mara kwa mara anapoona kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Mabadiliko ya sasa ni mwendelezo wa kuisika serikali yake ili kutimiza lengo la kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta mbalimbali.

Uteuzi huo wa mara kwa mara ulianza baada ya kuchukua madaraka ya urais Machi 19, 2021 baada ya aliyekuwa akishika nafasi hiyo, Dk. John Magufuli, kufariki dunia.

Mara kwa mara amekuwa akiweka bayana kwamba kuna baadhi ya watu hawaendani na kasi anayoitaka katika kuleta mabadiliko kwenye miradi ya maendeleo ili kuleta maendeleo ya wananchi katika ngazi mbalimbali.

Kwa maana hiyo, Rais amekuwa haliridhishwi ni baadhi ya wateule wake kuanzia ngazi ya wilaya na halmashauri ndiyo maana amekuwa akitoa mikeka ya mabadiliko, ukiwamo wa Jumapili ambao baadhi ya watu uteuzi wao umetenguliwa.

Hali hiyo inasadifu kauli aliyoitoa wakati akifunga Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwamba anaomba rai kuisuka serikali yake kutokana na aliyoyaona kwa baadhi ya wateule wake kusuasua kwenye utendaji wao.

Pamoja na kueleza hayo mara kwa mara, juzi Rais Samia alitoa ya moyoni juu ya yale yanayoendelea katika wizara mbalimbali, pale aliposema amechoka kuendekeza ugomvi wa baadhi ya mawaziri na manaibu wao.

Kwa hakika, kauli hiyo ya Rais ni nzito na imeonyesha kuwa hali si shwari katika wizara kadhaa na kwamba baadhi ya mawaziri na manaibu wao pamoja na makatibu wakuu na manaibu wao hawazungumzi na wengine wamekuwa wakigombana kila uchao.

Ni dhahiri kwamba kauli hiyo ya Rais Samia si ngeni licha ya kwamba imewekwa hadharani. Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa baadhi ya manaibu mawaziri kwamba wakuu wao (mawaziri) hawawapangii majukumu na kwamba kazi zote wamekuwa wakizifanya wao na kwamba hata zinapotokea safari mawaziri pekee ndio wanaokwenda na si manaibu wao.

Wateule wa Rais katika wizara, kwa maana ya mawaziri na naibu mawaziri, wanapaswa kutambua kwamba nafasi walizopewa ni dhamana na wanachotakiwa kufanya ni kutekeleza masuala ya kisekta yanayoangukia wizara zao kwa nia ya kumsaidia Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo ndio mkataba kati ya chama tawala na wananchi kupitia serikali iliyowekwa madarakani.

Kuna msemo kwamba nyumba inayojengwa ni moja sasa kwa nini kunyang'anyana fito? Ni vyema mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu wanapaswa kuacha tofauti zao pembeni ni kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuleta maendeleo yaliyokusudiwa badala ya kuendekeza ugomvi, chuki na visasi.

Rais Samia, kama alivyosema kwamba amechoka hadithi hizo zinazoonekana kutokuwa na mwisho kama hazitakemewa, kama alivyofanya, akiwa kiongozi mkuu wa nchi, asiwavumilie bali achukue hatua za kuwaondoa wote badala ya kuwahamisha au kumwondoa mmoja na mwingine kubaki. Watanzania hawataki hadithi za aina hiyo ambazo zimepitwa na wakati bali maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Karibu Lema utetee taifa lako, CHADEMA

**SHIRIKA** la Kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) linasema dunia ya leo inakabiliwa na viwango vikubwa vya watu waliokimbia makazi yao kuliko ambavyo imewahi kutokea katika historia.

UNHCR inasema wapo watu milioni 65.3 waliolazimika kuyahama makazi yao kutokana na vita, migogoro ya ndani hasa ya kisiasa, ukame au hali duni ya kiuchumi.

Suala la kukimbia ili kujinusuru na kuokoa maisha ni jambo linaloshuhudiwa Tanzania baada ya wanasiasa kadhaa hasa wa upinzani kukimbia kwa maelezo kuwa wanasalimisha maisha yao.

Wanaoshuhudiwa wakiishi ughaibuni ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, aliyehifadhiwa Ubelgiji baada ya kupigwa risasi zaidi ya 20 kutokana na kile anachoeleza kuwa ni kunyamazishwa asiendelee na harakati za kisiasa.

Mwingine ni mbunge wa zamani wa Arusha Mjini Godbless Lema. Aliyekimbilia nchini Canada, leo anarejea, akiwa miongoni mwa 'wakimbizi' wanaolalamika kukimbilia ughaibuni kutokana na sintofahamu za kisiasa.

Lissu amerejea na anaendeleza harakati za kisasa na sasa CHADEMA wanamsubiri Lema. Ujio wa wanasiasa hawa ni matokeo ya sera za usuluhishi na maridhiano zinazotekelezwa na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Ujio wa Lema ni chachu kwenye harakati za kuendeleza demokrasia kwa kuwa zinapotaja siasa za Tanzania na hata za nchi jirani hasa Kenya huwezi kukosa jina la Godbless Lema.

Umachachari, ujana na misimamo yake katika kusimamia hoja ndani na nje ya bunge pamoja na kushiriki harakati za kujenga upinzani imara na kutaka Tanzania yenye demokrasia, maridhiano na inayokubali mchango wa vyama vya upinzani, ni kati ya haiba zinazomweka mwanasiasa huyo kwenye orodha ya wapinzani mahiri.

Mashabiki, wapenzi wake na wanaofuatilia masuala ya kisiasa, wanamwelezea Lema kwamba sifa hizo ndizo zilimfanya aondoke nchini baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kuelekea ughaibuni kwa kile kilichoelezwa ni 'kujinusuru' kutokana na kile anachodai kuwa ni vitisho vya maisha yake.

Mwanasiasa huyo anawasili nchini leo huku akipokelewa na viongozi wote waandamizi wa CHADEMA, watakaoongozwa na Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe.

Lema ni kinara tena shujaa kuwa mstari wa mbele kuongoza maandamano na hoja za kupinga baadhi ya mambo yanayofanywa na Chama Cha Mapinduzi na harakati zake zimekiwezesha chama chake kuongoza Halmashauri ya Jiji la Arusha mwaka 2015-2020.

Misimamo yake imemweka matatani ikiwamo kukamatwa na polisi, kuwekwa mahabusu na kufunguliwa kesi za uchochezi mara kwa mara na wakati mwingine kuwa mtu anayesakwa na polisi.

Hata kuondoka kwake nchini kuelekea Canada, ilikuwa kama sinema kutokana na namna anavyosimulia hatari iliyokuwa inamkabili na familia yake na jinsi watu walivyosimama naye hasa wanasiasa wa nchi jirani ya Kenya.

Lema anarejea kwenye harakati za siasa za upinzani na kuendeleza demokrasia kukiwa na mambo mengi yaliyotokea ikiwamo kufunguliwa kwa mikutano ya hadhara na madai ya katiba mpya ambayo imekuwa agenda ya wengi.

Juhudi za kuweka mambo sawa na kuhakikisha Tanzania inakuwa na maridhiano ni mambo ambayo Rais Samia anayasimamia.

Anapenda kila mmoja ashiriki kuijenga Tanzania lakini wapinzani kama ambavyo wako kikatiba washiriki kwenye kazi ya kuisimamia, kuikosoa na kuishauri serikali na kuonyesha njia ili kufikia juhudi za kuijenga nchi imara.

Leman na Lissu wanaporejea tena kwenye majukwaa ya kisiasa la muhimu kujifunza na kudumisha ni kudumisha maridhiano na kukumbuka kuwa siasa si uadui, mawazo mbadala na kutofautiana ni jambo lililokuwapo tangu kuanza dunia.

Tena kuna ukweli kuwa haijawahi kutokea watu wote wakawaza pamoja, wakanuia moja, wakatenda na kufanana kwa kila hali, hii inamaanisha kuwa upinzani upo na mawazo mbadala hayaepukiki na huo ndiyo upinzani wa fikra na mitizamo.

# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

### (Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kwa ajili ya kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira. Maelezo ya Waombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:-

| S/No | Mwombaji | Anwani | Chanzo cha Maji | Miundombinu | Maelezo ya Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tunduru | SLP 275, Tunduru RUVUMA baruapepe:mdtunduru@maji.go.tz | Chemchem ya Nanjoka , visima virefu saba na mto wa Mlingoti | Matenki ya maji 12 yenye jumla ya mita za ujazo 650. Mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 73km na vilula 6. | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Tunduru. |
| 2. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tunduma | S.L.P127, Tunduma - SONGWE | Visima virefu 7, vilivyopo maeneo ya Ikulu, Sogea, Tazara, Mamboleo, Maporomoko,Makambini na Mahakama. | Matenki ya maji 10 yenye jumla ya mita za ujazo 699. Mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 49km na vilula 19 | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Tunduma |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

**Mkurugenzi Mkuu**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi
S. L. P 2857, Dodoma.
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA LOLIONDO (LOLIONDO WSSA)

Mnamo tarehe 30 Desemba 2022 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Loliondo (Loliondo WSSA). Majedwali Na 1 hadi 3 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Loliondo WSSA.

**Jedwali 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 2,500 | 2,500 | 2,500 | 2,500 |
| Taasisi | 2,500 | 2,500 | 2,500 | 2,500 |
| Biashara | 2,500 | 2,500 | 2,500 | 2,500 |
| Magati | 2,500 | 2,500 | 2,500 | 2,500 |

**Jedwali 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shlingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Wateja Wote | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

**Jedwali 3: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani<br>Taasisi<br>Biashara<br>Viwanda | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | | |

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Maji Loliondo, bei na ada zinazopendekezwa zitawezesha mamlaka kutekeleza shughuli zilizoainishwa katika mpango kazi wake kwa kipindi cha kuanzia 2022/23 hadi 2024/2025 na hivyo kuhakikisha uendelevu katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira. Hasa, ushuru na ada zinazopendekezwa zitawezesha kuongezeka kwa huduma, kupunguza maji yasiyo ya mapato, kuongezeka kwa uzalishaji wa maji na kuboresha uwezo wa kitaasisi wa shirika.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya Alhamisi, tarehe 9 March 2023, katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Loliondo Mjini kuanzia saa 4:00 asubuhi kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la Watumia Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo chini wakati wowote hadi tarehe 16 Machi 2023. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Loliondo WSSA yanaweza kupatikana kwenye ofisi za Makao Makuu ya EWURA zinazopatika katika Jengo la EWURA, Medeli Magharibi, Dodoma au Ofisi za EWURA Kanda ya Kaskazini zilizopo Ghorofa ya Pili, Jengo la PSSSF, Jirani na Kibo Palace Hotel, Arusha Mjini au kwenye Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Loliondo zilizopo Loliondo Mjini.

**Mkurugenzi Mkuu**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi
S. L. P 2857, Dodoma.
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MOMBO

Mnamo tarehe 02 Januari 2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za huduma za maji safi na usafi wa mazingira kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo. Majedwali Namba 1 hadi 4 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo.

**Jedwali Na. 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 395 | 1,000 | 1,100 | 1,200 |
| Taasisi | 390 | 1,000 | 1,100 | 1,200 |
| Biashara | 400 | 1,100 | 1,100 | 1,200 |
| Viwanda | 500 | 1,290 | 1,400 | 1,500 |
| Magati | 500 | 1,300 | 1,400 | 1,500 |

**Jedwali Na 2: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi kwa Mwezi)**

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 4,500 | 6,000 | 7,500 | 8,000 |
| Taasisi | 16,500 | 17,000 | 17,500 | 18,000 |
| Biashara | 9,500 | 10,000 | 11,000 | 12,000 |
| Viwanda | 10,000 | 12,000 | 13,000 | 14,000 |
| Magati | 12,000 | 13,000 | 14,000 | 15,000 |

**Jedwali Na. 3: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa 2021/22 | Ada zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani<br>Taasisi<br>Biashara<br>Viwanda | Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvukazi kama ilivyoainiswa katika Sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji 2013 | Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvukazi kama ilivyoainiswa katika Sehemu ya 26 ya Kanuni za Maji 2019 | | |

**Jedwali Na. 4: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shlingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo imeeleza kuwa bei zilizopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kuboresha ufanisi katika utoaji huduma endelevu. Bei zinazopendekezwa zimezingatia mabadiliko ya kiuchumi yananayoathiri sekta ya maji, mabadiliko ya mahitaji ya udhibiti na utekelezaji wa mpango wa biashara wa Mamlaka ya Maji Mombo.

Tangazo hili limetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA Sura ya 414, kinachoitaka EWURA kutoa tangazo la taftishi ili kukusanya maoni kutoka kwa wadai ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali (EWURA GCC), Baraza Ushauri la Watumiaji wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC), Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo na Umma kwa ujumla kuhusu bei zinazopendekezwa. Kama sehemu ya taftishi, kutakuwa na mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau utakaofanyika siku ya Alhamisi, tarehe 9 Machi 2023 katika Ukumbi wa Bugati Mombo kuanzia saa nne asubuhi.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo juu wakati wowote hadi tarehe 13 Machi 2023. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo; yanaweza kupatikana kwenye ofisi za Makao Makuu ya EWURA zinazopatika katika Jengo la EWURA, Medeli Magharibi, Dodoma au Ofisi za EWURA Kanda ya Kaskazini zilizopo Ghorofa ya Pili, Jengo la PSSSF Plaza, Karibu na Kibo Place Hotel, Arusha Mjini au kwenye ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo.

**Mkurugenzi Mkuu**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi
S. L. P 2857, Dodoma.
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA DODOMA (DODOMA WSSA)

Mnamo tarehe 26 Januari 2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (Dodoma WSSA). Majedwali na. 1 hadi 6 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Dodoma WSSA.

**Jedwali Na. 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Kundi la Wateja | Matumizi ($m^3$) | Bei ya Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 0-5 | 1,170 | 1,376 | 1,571 | 1,632 |
| | 6-10 | 1,250 | 1,990 | 2,210 | 2,495 |
| | 11-30 | 1,260 | | | |
| | Zaidi ya 30 | 1,300 | | | |
| Taasisi | | 1,620 | 1990 | 2,210 | 2,495 |
| Biashara | | 1,660 | 2,010 | 2,319 | 2,510 |
| Viwanda | | 1,660 | 2,010 | 2,319 | 2,510 |
| Magati | | 600 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| Wateja wa Jumla | | 1,800 | 2,040 | 2,060 | 2,100 |

**Jedwali 2: Tozo ya Majitaka ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Mwezi)**

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Inayopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Wateja Wote | Asilimia 40 ya gharama ya maji | Asilimia 50 ya gharama ya maji | Asilimia 50 ya gharama ya maji | Asilimia 50 ya gharama ya maji |

**Jedwali 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shlingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 15,000 | 25,000 | 30,000 | 35,000 |
| Taasisi | 15,000 | 50,000 | 55,000 | 65,000 |
| Biashara | 15,000 | 50,000 | 55,000 | 65,000 |
| Viwanda | 15,000 | 50,000 | 55,000 | 65,000 |
| Magati | 15,000 | 25,000 | 30,000 | 35,000 |

**Jadwali 4: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani<br>Taasisi<br>Biashara<br>Viwanda | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | | |

**Jedwali 5: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Uondoaji wa Majitaka (Shilingi kwa Tripu)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2022/23 |
| Majumbani | 60,000 | 120,000 | 135,000 | 150,000 |
| Wengine | 75,000 | 125,000 | 140,000 | 155,000 |

**Jedwali 6: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kumwaga Majitaka kwenye Mabwawa ya Dodoma WSSA (Shilingi kwa Tripu)**

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Wateja Wote | 1,000 | 2,000 | 2,500 | 3,000 |

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Maji Dodoma, bei na ada zinazopendekezwa zitawezesha mamlaka kukidhi ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo na uwekezaji. Zaidi ya hayo, Mamlaka imeeleza kuwa mapendekezo ya marekebisho ya bei yatawezesha utekelezaji wa shughuli zilizowekwa katika Mpango Biashara wa Mwaka 2023/24 – 2025/26, na hivyo kuhakikisha uendelevu katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2)(b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya Alhamisi, tarehe 6 Aprili 2023, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma Mjini kuanzia saa 4:00 asubuhi kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la Watumia Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo juu wakati wowote hadi tarehe 9 Aprili 2023. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Dodoma WSSA yanaweza kupatikana kwenye ofisi za Makao Makuu ya EWURA zinazopatika katika Jengo la EWURA, Medeli Magharibi, Dodoma au kwenye Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma zilizopo Dodoma Mjini

**Mkurugenzi Mkuu**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi,
S. L. P 2857, Dodoma.
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

# Katibu mkuu ataja mbinu ufanisi ukusanyaji kodi ya pango la ardhi

**Na Anthony Ishengoma,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Sanga, ameahidi kufanya mabadiliko makubwa ya mfumo wa ukusanyaji mapato yatokanayo na pango la ardhi kama ilivyo mifumo ya kisasa inayotumiwa na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira nchini.

Sanga alisema hayo jana wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya ofisi kati yake na mtangulizi wake, Dk. Alla Kijazi, baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuongoza wizara hiyo.

"'Ili kuwa na mafanikio makubwa ni lazima tujue idadi ya wamiliki wa ardhi nchini kwa kuwaingiza kwenye mifumo ili kujua kiwango cha mapato yatokanayo na kodi ya ardhi hapa nchini," alisisitiza Sanga.

Akitoa uzoefu wake katika mifumo ya ukusanyaji mapato kupitia Wizara ya Maji na mamlaka zake, Mhandisi Sanga alisema walifanikiwa kuwa na mifumo imara baada ya kuachana na mifumo kutoka nje ya nchi na kuwaamini wataalamu wa ndani. Alisema wataalamu wa ndani wametengeneza mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ya maji katika mamlaka za maji.

Kwa muktadha huo, Sanga alihimiza kutumia wataalamu wa mifumo ya ndani na kuamini watendaji wengine wa sekta ya ardhi kwa kuwapa nafasi ili kuonesha uwezo wao huku akibainisha kuwa yeye ana tabia ya kuamini watu anaofanya nao kazi.

Naye Katibu Mkuu anayemaliza muda wake, Dk. Allan Kijazi, aliwataka watendaji wa Wizara ya Ardhi kuendelea kufanya kazi kwa karibu na kiongozi huyo mpya ili kuendeleza kazi kubwa ambayo yeye na wenzake wamekuwa wakiendelea nayo hadi sasa wakati anamaliza muda wake.

Dk. Allan Kijazi aliwataka wajumbe wa menejimenti ya wizara kusaidia viongozi wapya wizarani ili kukabiliana na changamoto zilizoko hususani migogoro ya ardhi kwa kuwapitisha katika yale ambayo wameshayafanyia kazi na yale ambayo wataendelea kuyafanyia kazi na hatimaye kupata suluhisho la kudumu katika juhudi za kutokomeza migogoro hiyo.

Kijazi aliongeza kuwa tayari wizara imeshaanza kufanyia kazi migogoro ya ardhi na kwa kuanzia ilianzia katika mikoa yenye migogoro sugu na tayari kazi hiyo imekamilika katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma na litaendelea kwa mikoa ya Mwanza na Arusha.

Kuhusu makusanyo ya kodi ya pango la ardhi, Dk. Kijazi alisema mpaka sasa wastani wa ukusanyaji mapato ya ardhi ni kwa asilimia 60 tu, hivyo kumtaka Sanga kuboresha namna ya kuingiza wamiliki wa ardhi katika mifumo ili kulipa kodi ya serikali kama inavyotakiwa.

Pamoja na Naibu Katibu Mkuu wake, Lucy Kabyemela, mapema jana asubuhi waliwasili makao makuu ya wizara eneo la Mtumba na kupokewa kwa shangwe na watumishi wa wizara tayari kwa kuanza kazi baada ya uteuzi wao na Rais Samia hivi karibuni.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**TAARIFA KWA UMMA**

**Kusudio la Kufuta Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Wafanyabiashara Wasio na Sifa za Kuendelea Kusajiliwa katika VAT**

Kwa mujibu wa **Kifungu 28** na **29 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 (Rekebisho la Mwaka 2019),** wafanyabiashara waliotimiza vigezo vya kusajiliwa katika Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), wanatakiwa kuomba usajili huo kwa Kamishna Mkuu. Moja ya vigezo vya kusajiliwa katika VAT ni kuwa na mauzo kwa mwaka, yanayozidi kiwango cha chini kilichowekwa na **Kanuni ya 14 ya Kanuni za VAT za mwaka 2015** cha **Shilingi Milioni Mia Moja.**

Tathmini iliyofanyika kupitia kumbukumbu zetu za usajili wa VAT imebainisha kuwa, baadhi ya walipakodi waliosajiliwa katika VAT, wamepoteza sifa za kuendelea kuwa katika usajili ikiwa ni pamoja na biashara zao kutofikisha mauzo ya milioni mia moja kwa mwaka. Ili kuimarisha usimamizi mzuri katika VAT, Kamishna Mkuu anakusudia kutumia mamlaka aliyokasimiwa chini ya **Kifungu cha 41 cha Sheria ya VAT**, kuwafutia usajili walipakodi wote wenye mauzo chini ya kiwango tajwa, pamoja na wale waliopoteza sifa zilizoainishwa chini ya **Kifungu cha 29 cha Sheria ya VAT. Hata hivyo, kusudio hili halilengi kumuondolea mlipakodi wajibu wake wa kulipa kodi au kuwasilisha ritani za kodi za kipindi cha nyuma kwa walipakodi wanaotarajiwa kufutiwa usajili wa VAT.**

Kutokana na ufafanuzi huu, tunawajulisha kuwa **orodha kamili ya majina ya walipakodi wanaotarajiwa kufutiwa usajili wa VAT imewekwa kwenye tovuti ya TRA (www.tra.go.tz).** Mlipakodi yeyote mwenye pingamizi juu ya maamuzi ya Kamishna Mkuu, anatakiwa kuwasilisha pingamizi lake, akielezea sababu za kwanini asifutiwe usajiliwa VAT. Pingamizi ziwasilishwe katika **Ofisi za TRA kwa Meneja wa Mkoa husika** na **ziwasilishwe ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya notisi hii.** Baada ya siku 30 zilizowekwa kupita, Mamlaka itaendelea na zoezi la kufuta usajili wa VAT.

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo

| | |
|---|---|
| **Tovuti:** | www.tra.go.tz |
| **Namba ya Bure:** | 0800 750 075 au 0800 780 078 |
| **WhatsApp:** | 0744 23 33 33 |
| **Barua Pepe:** | huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz |

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Kidatah

A.J. Kidata
Kamishna Mkuu


# Serikali yamwaga pesa uboreshaji barabara

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imefanya maboresho makubwa kwenye miundombinu ya barabara nchini kwa kuongeza fedha za kugharamia ujenzi na matengenezo ya barabara, imeelezwa.

Meneja wa Mfuko wa Barabara Tanzania, Eliud Nyauhenga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na ujumbe kutoka Mfuko wa Barabara Zanzibar uliomtembelea ofisini kwake mtaa wa Ammar, jijini Dodoma.

"Kuanzia mwaka wa fedha 2021/22, serikali imekuwa ikitenga zaidi ya Sh. bilioni 440 kila mwaka mahususi kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara za mijini na vijijini. Hatua hii imesababisha kuimarika kwa kiwango kikubwa kwa mtandao wa barabara za vijijini.

"Hii ni pamoja na kufungua barabara nyingi ambazo zilikuwa hazipitiki hapo awali. Maboresha haya yanawawezesha wananchi kufikia na kunufaika na huduma za kijamii na kiuchumi zinazopatikana kutokana na miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali," alisema.

Nyauhenga aliuambia ujumbe huo kuwa makusanyo ya fedha za kugharamia matengenezo ya barabara yameongezeka kwa asilimia 27 kutoka Sh. bilioni 806.7 mwaka wa fedha 2019/20 hadi Sh. bilioni 1,027 mwaka wa fedha 2021/22.

Pia alisema kwa miaka yote mitatu iliyopita, serikali imekuwa ikitoa fedha zote za kugharamia matengenezo ya barabara kama zinavyoidhinishwa na Bunge na kwamba hatua hiyo imewezesha kutekeleza kazi nyingi za matengenezo ya barabara, hivyo kulinda thamani ya uwekezaji wa serikali kwenye miundombinu na kuwawezesha watumiaji wengi wa barabara kupata huduma nzuri za usafiri na usafirishaji.

Alisema serikali ilianzisha Mfuko wa Barabara Tanzania mwaka 2000 kupitia Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta Sura ya 220 ili kugharamia kikamilifu matengenezo ya barabara zote za Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Nyauhenga, chanzo kikuu cha mapato ya mfuko huo ni tozo za mafuta ambazo ni Sh. 363 kwa kila lita ya dizeli na petroli, tozo kwa magari ya kigeni yanayotumia barabara nchini pamoja na faini zinazotozwa kutokana na uzidishaji uzito wa magari.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuandaa Mwongozo wa Utumiaji Barabara Zanzibar, CPA Bakari Rashid, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeunda kamati hiyo ili kuboresha matumizi ya barabara za Zanzibar na kwamba kamati yake tayari imetembelea barabara zote za Unguja na Pemba kabla ya kuamua kutembelea Mfuko wa Barabara Tanzania.

Naye Omar Makame, Mwenyekiti wa Kamati ya Mapitio ya Mpango Mkakati wa Mfuko wa Barabara Zanzibar, alimshukuru Nyauhenga kwa kukutana nao kuwa kamati zao zimejifunza mambo mengi kuhusu uendeshaji wa mfuko wa barabara na kwamba Mfuko wa Barabara Zanzibar utaendeleza ushirikiano madhubuti uliopo baina ya mifuko hii miwili nchini.



# TGC yasaidia kupunguza kiwango cha usafirishaji wa madini nje

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI imesema kuwapo kwa Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC), kumesaidia kupunguza kiwango cha usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi na kimezalisha wataalamu wabobezi wa uongezaji thamani na uthaminishaji.

Kutokana na kuwapo kwa wataalamu hao wameisaidia serikali kukusanya kodi inayotokana na thamani halisi ya bei ya madini duniani.

TGC ni kituo pekee katika ukanda wa Afrika Mashariki kinachotoa mafunzo ya uongezaji thamani madini katika nchi za ukanda huo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kaimu Mratibu wa TGC, Daniel Kidesheni, alisema kituo hicho kimezisaidia nchi mbalimbali za Afrika kuwapatia mafunzo vijana ambayo yamewasaidia kuongeza thamani ya madini katika nchi zao.

Alisema kituo hicho kinapokea wanafunzi kutoka nchi za Kenya, Uganda, Ufaransa na nchi nyingine ambazo wanakwenda kupata mafunzo ya utambuzi wa aina za madini katika kituo hicho.

Alisema hapa nchini kituo hicho kimewanufaisha vijana wengi kwa kujiajiri kupitia kazi za usonara na kujikwamua kiuchumi wao wenyewe na familia zao.

"TGC kina manufaa makubwa kwa Tanzania kwa kuwa vijana wengi wanapata mafunzo ya namna ya utofautishaji wa madini,"alisema Kidesheni.

Alisema kutokana na umuhimu wa kituo hicho sasa hivi wananchi wengi wanajua rasilimali za nchi ikiwamo kufahamu namna ya kuongeza thamani bidhaa zitokanazo na madini tofauti na kama ilivyokuwa awali.

Mmoja wa wakufunzi wa TGC, Erick Mpesa, alisema mafunzo hayo yanawasaidia wachimbaji kutambua aina mbalimbali za madini kabla hayajaingia sokoni.

Alisema uzalishaji wa wataalamu katika kituo hicho kumewasaidia wachimbaji kujua aina ya madini na thamani yake yanapochimbwa tofauti na ilivyokuwa mwanzoni.

"Kituo hiki kimesaidia wachimbaji pamoja na wafanyabiashara kujua aina za madini, kwa kuwa mwanzo wachimbaji walikuwa wanaweza kuuza madini kwa bei ya hasara kutokana na kutokujua thamani na aina ya madini hayo,"alisema Mpesa.

Naye Carren Laswai, mwanafunzi anayesoma kituo hapo, alisema kituo hicho kimewasaidia vijana kujiajiri wenyewe baadaa ya kuhitimu mafunzo yao.

Licha ya kuzungumza hayo ameiomba serikali kutatua baadhi ya matatizo ya kituo na mabadiliko ya teknolojia kwenye tasnia hiyo.

## DC awaomba viongozi kukemea matukio ukatili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda, amewaomba viongozi wa mila wa jamii ya Wamasai (Malaigwanani), kukemea matukio ya ukatili yanayoibuka hivi sasa.

Kaganda alitoa ombi hilo jana jijini Arusha alipokutana na viongozi wa mila katika eneo la Chuo cha Ufundi Arusha(ATC), ambalo jamii ya Wamasai hulitumia kwa ajili ya kufanya mambo ya mila ikiwamo kupata baraka.

Alisema endapo viongozi wa mila watatoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake, watoto na makundi mengine matukio ya ukatili yatapungua.

"Sijisikii vizuri kusikia matukio mbalimbali ya ukatili yanatokea katika wilaya yangu, naomba viongozi wa mila tushirikiane katika hili, lakini nawapongeza kwani kabila la Wamasai ukweli ni kabila lenye kudumisha mila na tamaduni," alisema.

Aidha, aliwaomba pia kushirikiana na serikali kuhakikisha utandawazi kupitia teknolojia ya simu za viganjani uwasaidie vijana kupata maendeleo.


Pamoja na maombi hayo, Kaganda alitoa zawadi ya viti zaidi ya 20 vitakavyowawezesha viongozi hao kukaa wakati wanapofanya mikutano yao pamoja na mablanketi kwa ajili ya viongozi hao kujifunika wakati wa baridi.

Katibu wa Malaigwanani, Amani Lukumay, alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kufika katika eneo hilo kwa ajili ya kujadili matatizo yao.

Kuhusu suala la utandawazi unaoharibu maadili kwa jamii alisema watashirikiana na serikali ili kudhibiti hilo kwa ustawi wa taifa.

Tamasha hilo limelenga kutangaza utalii wa kitamaduni nchini kwa ajili ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan, katika kukuza sekta ya utalii.





# Matukio mauaji yaripotiwa Kagera, Muleba kinara

**Na Waandishi Wetu,**
KAGERA

MATUKIO 190 ya mauaji yametokea mkoani Kagera kwa mwaka 2022, huku Wilaya ya Muleba ikitajwa kuwa ni kinara wa matukio hayo.

Pia imetajwa kuwa kati ya matukio hayo wivu wa mapenzi ndiyo chanzo cha mauaji hayo.

Kamishna Msaidizi wa Polisi mkoani Kagera, Maketi Msangi, aliyasema hayo wakati akiongea na viongozi mbalimbali wakiwamo wazee, watendaji wa kata pamoja na viongozi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Bukoba.

"Mkoa wetu ndiyo unaongoza kwa mauaji ambapo kwa takwimu Wilaya ya Muleba ndiyo inayoongoza kwa vitendo hivi. Yameripotiwa matukio 190 kwa mwaka 2022, Wilaya ya Muleba ina matukio 40, Ngara matukio 36 na Bukoba matukio 30."

Kamishna wa Polisi Jamii Jeshi la Polisi Tanzania, Faustine Shingile, alisema kuwa matukio ya mauaji yamekuwa yakipanda na katika kipindi cha Januari mwaka huu yametokea matukio 35. "Kidogo mkoa wetu ulichafuka sana baada ya matukio ya mauaji kupanda, mwaka jana tulikuwa hapa ila tunaona mauaji bado yanazidi kupanda ukiangalia kwa mwaka huu. Januari tu yameishatokea matukio 35," alisema.

Aliongeza kuwa uchunguzi unapofanyika kwa asilimia kubwa chanzo kimebainika kuwa wivu wa mapenzi, hivyo kuamua kuanzia katika mkoa huo kwa kukutana na viongozi wa mbalimbali ili kujua chanzo na kudhibiti vitendo hivyo.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Mstaafu, Engelbert Kiondo, aliwasihi viongozi wa dini kuzidisha mahubiri yenye ubunifu yanayokemea vitendo hivyo.

"Taasisi hizi za kidini zinatakiwa kuangalia upya njia mpya za utoaji wa mafundisho yanayokemea vitendo hivyo, mnatakiwa muwafuate hata waumini wenu majumbani kukemea vitendo hivyo kwani unakuta wakati wengine mnaowapatia elimu kila siku wale wale, wengine hawaji kanisani wala msikitini sasa," alisema.

Mmoja wa wazee aliyekuwapo katika mkutano huo, Mzamidu Hassan alipendekeza viongozi za usalama kufanya semina za mara kwa mara na ziwe shirikishi kwa wananchi.

Mwakilishi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) wilayani Bukoba, Naomi Kajuni, alisema endapo jamii ikikubali kubadili mtazamo na kujifunza jinsi mikoa mingine ilivyofanikiwa kukabili matukio ya mauaji itasaidia kupunguza matukio hayo.

Alisema migogoro mingi inatokea kwenye ndoa kwa kukosa maadili na kusababisha ukatili, kwamba hakuna muda wa kuwalea watoto katika misingi ya kumwamini Mungu.

**Imeandaliwa na Titus Mwombeki na Restuta Damian**




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha madumu ya mafuta ya dizeli lita 780 yaliyoibwa kwenye mradi wa reli ya kisasa SGR baada ya kuyakamata wilayani Kahama juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# TASAF yagawa mbuzi kwa kaya 106 Mwanza

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia Mpango wa Kuinua Kaya Maskini wilayani Ilemela umetoa mbuzi 424 wenye thamani ya Sh. milioni 36.04 kwa kaya 106 kwa lengo la kuzinusuru kaya hizo na umaskini.

Kaya hizo ni kutoka Kata ya Nyamh'ongolo na Sangabuye zilizopo wilayani Ilemela ambazo ni wanufaika wa mradi unaofadhiliwa na Muungano wa Nchi Wasafirishaji wa Mafuta ya Petroli (OPEC) huku wakitakiwa kuhakikisha wanatunza mifugo hiyo ili iweze kuzaliana na kuwasaidia kiuchumi.

Akizungumza wakati wa kuwakabidhi mbuzi hao, Mratibu wa TASAF Wilaya ya Ilemela, Leonard Robert, alisema wanayo matarajio kuwa uchumi wa kaya hizo unaenda kuimarika kupitia mradi huo.

Aliwataka walengwa wa TASAF wanawatunza mbuzi hao ili waweze kuzaliana na baadaye waje kuwasaidia katika utatuzi wa changamoto za kiuchumi katika kaya zao ikiwa ndio lengo la mradi huo.

"Uchumi wa kaya unaenda kuimarika na changamoto zinaenda kupungua ambapo kila kaya itakuwa na jukumu la kuwatunza na kuwalinda,"alieleza Leonard.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Leah Mabula, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo na kuahidi kuwatunza mbuzi hao ili waweze kuzaliana ili familia yake iweze kujikomboa kiuchumi.

Diwani wa Kata ya Nyamh'ongolo, Andrea Nginila, alieleza kuwa mradi huo utaenda kuleta tija kwa wananchi wake kwa kuwaondolea umaskini.

# Mratibu Elimu afariki dunia kwa kugongwa na gari

**Elizabert Seleman,**
SENGEREMA

MRATIBU Elimu Kata ya Kasungamile wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Isack Sayi, amefariki dunia baada ya kugongwa na gari aina ya lori.

Gari hilo ambalo hakikufahamika namba zake za usajili lilimgonga mratibu huyo ambaye alikuwa akiendesha pikipiki na kufariki dunia papo hapo.

Wakizungumzia ajali hiyo, mashuhuda wa waliokuwapo (hawakutaja majina yao) walisema gari hilo lilikuwa likitokea jijini Mwanza kuelekea mkoani Geita.

Walisema marehemu alikuwa akitokea Sengerema kwenda nyumbani kwake Kata ya Nyampande na akiwa barabara alihama upande wake na kuingia upande wa dereva wa gari hilo.

Baadhi ya watumishi waliowahi kufanya kazi na marehemu walisikitishwa kutokea kwa tukio hilo wakisema kuwa marehemu ameacha pengo.

Ndugu wa marehemu walisema msiba huo ni pengo kwa familia kwani alikuwa tegemeo lao katika kupata mahitaji muhimu.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema watu ambao wanatumia vyombo vya moto wanatakiwa kuwa makini muda wote wanapokuwa barabarani.

Ngaga alisema tayari dereva wa gari hilo linalodaiwa kusababisha ajali hiyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi wilayani Sengerema.

Ngaga alisema msiba huo umeacha pengo kwa serikali kwa kuwa marehemu alikuwa tegemeo, kwamba marehemu alizikwa juzi nyumbani.

UVCCM yaanza mwaka kwa kishindo, yaanzisha mpango wa kurejea darasani

Ukurasa 12



Ukurasa 14



# siasa

JUMATANO MACHI 1, 2023
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

## SHAMIM KHAN Mbunge, waziri aliyeacha nyayo kuinua wanawake kwenye uchumi na biashara

WANAHABARI WATAKA SMZ IWAPE RAHA

# Ni kuwaondolea Sheria ya Usajili wa Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu

■ Inaongeza hofu, kuwapa polisi kazi za 'kubinya media'

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

LICHA ya Zanzibar kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa ya haki za binadamu na uhuru wa kutoa maoni na kupata habari, wanahabari wanadai sheria kandamizi visiwani ni mwiba unaoongeza hofu na woga kwa waandishi.

Aidha, pamoja na katiba ya mwaka 1984 ambayo ibara ya 18 inaeleza uwepo wa uhuru wa kupata habari, sheria zinazobinya uhuru huo zinakwamisha wananchi kupata na kufurahia haki hiyo.

Pamoja na katiba kueleza kuwa uhuru wa kujieleza na kupata habari ni haki ya msingi, sheria namba tano ya Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu ya 1988 ina baadhi ya vifungu vinavyokwamisha uhuru huo, wanaeleza wadau.

Kifungu cha 18 (1) cha katiba ya Zanzibar, kinaeleza kuwa: "bila ya kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa mawazo yake na kutafuta, kupokea na kutoa habari kupitia chombo chochote, bila ya kujali mipaka ya nchi na pia ana uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa."

Kadhalika, kifungu cha 2 cha katiba kinasema "Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Kutokana na sheria hiyo ya Usajili wa Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu ya mwaka 1988 kuathiri uhuru wa habari na haki ya kujieleza wadau na waandishi wa habari Visiwani, wanataka ifanyiwe marekebisho ili kwenda na wakati uliopo.

Jabir Idrissa, mwandishi wa habari mwandamizi anasema kifungu cha 27(1),(2) cha sheria hiyo kinampa mamlaka polisi kukamata magazeti na kupekua majengo, jambo ambalo linaweza kutafsirika kama ni kuingilia uhuru wa habari.

Aidha, anasema kifungu kidogo (2) cha sheria hiyo kinaeleza kuwa hakimu yeyote anaweza kwa hati, kumruhusu ofisa yeyote wa polisi wa cheo cha mkaguzi au cha juu zaidi akiwa na msaada au bila ya msaada, kuingia na kupekua sehemu yeyote ambayo kwa maoni yake anadhani kwamba kuna gazeti lililochapwa kinyume na sheria hiyo.

Idrissa anasema kutokana na kasoro hizo katika sheria hiyo, inahitaji kufanyiwa marekebisho ili waandishi wa habari wafanye kazi zao kwa weledi bila ya kuingiliwa.

Shifaa Said, Ofisa Mwandamizi wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) anasema, kuna baadhi ya vifungu katika sheria ya hiyo siyo rafiki kwa wanahabari, hali inayosababisha baadhi yao kufanya kazi kwa woga na hofu.

"Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA Zanzibar) kwa kushirikiana na Shirika la Internews, wanakutana na wadau mbalimbali wa habari kujadili kasoro zilizomo ndani ya sheria hiyo na kutoa maoni yao, ili maoni hayo yawasilishwe serikalini kufanyiwa maboresho ili kuwa na sheria rafiki kwa waandishi," anasema Shifaa.

Zaina Abdallah Mzee, Mratibu wa Mradi wa Boresha Habari unaotekelezwa na Internews Tanzania kwa kushirikiana na TAMWA, anasema wameamua kuungana kupaza sauti ili kuwa na sheria bora ambazo haziathiri uhuru wa habari na ule wa kujieleza.

Anaeleza kuwa licha ya kasoro zilizopo katika sheria hiyo lakini zipo sheria nyingine ambazo zinakandamiza uhuru wa habari.

Aidha, anawataka waandishi wa habari na wadau wa habari visiwani Zanzibar kuibua sheria zote kandamizi dhidi ya habari na huru wa kujieleza na kupeleka maoni yao serikali ili zifanyiwe marekebisho, kama ambavyo serikali iliahidi.

"Suala la kupata, kusambaza habari lipo kikatiba zaidi, sasa kama sheria imetungwa inakinzana na haki hiyo, haina nafasi kwa sasa hivyo inahitaji kufanyiwa marekebisho mara moja,"anasema.



Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, akiwa kwenye mkutano na wadau wa habari. **PICHA: MWANDISHI WETU**

Salma Said, Katibu wa Chama cha Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA), anasema kifungu hicho kinapaswa kufanyiwa kazi haraka, kwa sababu kinampa mamlaka makubwa polisi, wakati zipo taasisi za kihabari zinazopaswa kusimamia jambo hilo.

Anaongeza kuwa kuwepo kwa mamlaka hayo kutawawezesha wanahabari, wauzaji, wasambazaji na kampuni kupata hofu kwa kuhofia kukamatwa na wengine kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

"Kama kuna mamlaka inahisi gazeti limeaandika vibaya au limekwenda kinyume na sheria za habari, ni vizuri kufuata taratibu za kisheria na sio kuwakamata moja kwa moja au kuwavamia," anasema.

Dokta Mzuri Issa, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, anasema mamlaka ya polisi inawajibika kulinda raia na mali zao na amani ya nchi, hivyo majukumu yaliyomo katika kifungu 27(1)(2) yanapaswa kufanyiwa maboresho.

Shadida Ali, Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) ofisi ya Zanzibar, anasema, kifungu hicho hakipo sawa na kinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Anasema sheria inayompa nguvu ofisa wa polisi uwezo wa kukamata na kufanya upekuzi, ni kipimo kikubwa cha ukiukaji wa uhuru wa habari nchini.

Hata hivyo, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, anawahakikishia waandishi na wadau wa habari azma ya serikali ya kuifanyia marekebisho sheria hiyo kwa ujumla wake.

"Najua mna hamu ya kuona muswada wa sheria ya habari unawasilishwa Baraza la Wawakilishi lakini niwaambie kwamba hatupo kimya, tunaendelea kuufanyia kazi na hivi karibuni utawasilishwa," anasema.

Anasema muswada huo umejumuisha mapendekezo yote ya wadau yenye maslahi kwa jamii ya Wazanzibari na Watanzania na kuwaomba, kuwa na subira kwani hawatasita kurudi kwao wakiona kuna haja ya kufanya hivyo.

"Sheria ina pande mbili inatoa fursa na pia inatoa wajibu, tunayo haki ya kukosoa lakini nadhani tungejikita katika kujenga hoja kuliko kukosoa zaidi serikali," anasema Tabia.



Baadhi ya viongozi wa CCM wakiwa kwenye kikao kilichohutubiwa na Mwenyekiti Mkoa, Twaiba Mpako. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

# UVCCM yaanza mwaka kwa kishindo, yaanzisha mpango wa kurejea darasani

## •Kila mmoja kufunzwa uongozi, uadilifu

**Na Sabato Kasika**

VIONGOZI wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), wamekumbushwa kutekeleza kwa vitendo ahadi ya chama inayowaagiza 'kujielimisha kwa kadri ya uwezo wangu na kuitumia elimu yangu kwa faida ya wote.'

Ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Lindi, Twaiba Mpako, anayeagiza viongozi wa vijana wa chama hicho kwenda darasani kusoma elimu ya uongozi.

Ni Februari 17, 2023, anatoa maagizo hayo, katika kikao cha Baraza la UVCCM, mkoa wa Lindi, kilichofanyika mjini Liwale, ajenda kuu ikiwa ni kukamilisha safu ya uongozi wa UVCCM ngazi ya mkoa.

Ukamilishaji huo wa safu ya uongozi, unahusisha uchaguzi wa wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji Mkoa na kumthibisha Katibu Hamasa na Chipukizi wa Mkoa wa Lindi, ndipo anapotoa maelekezo hayo.

Twaiba anaanza kwa kusema, viongozi wa UVCCM, hawatakiwi kuingiliana katika majukumu na kwamba kila mmoja wao ni vyema aheshimu majukumu ya mwezake, ili kuepusha migogoro ndani ya jumuiya hiyo.

"Hivyo, ninaagiza viongozi wa kata zote mhudhurie madarasa ya elimu ya uongozi, ambayo yatapangwa kwenye kila wilaya, ili mjue kazi zenu ndani ya jumuiya na chama kwa ujumla," anasema Twaiba

Aidha, Mwenyekiti wa UVCCM mkoa, anawataka viongozi hao kuwa na kanuni za umoja huo, kuzisoma na kuelewa zaidi majukumu yao ikiwa ni njia mojawapo na kuendelea kuimarisha umoja ndani ya jumuiya hiyo.

"Kila kiongozi akitambua majukumu yake na kuheshimu ya mwezake, tutaepusha migogoro, tutafanya kazi kwa ufanisi na umakini zaidi kuitumikia CCM, hivyo hudhurieni madarasa ya elimu ya uongozi," anasema.

> "Tutatoa ushirikiano na ushauri, ili Umoja wa Vijana Mkoa wa Lindi, uzidi kuimarika, ila madarasa mengi ya uongozi yatafanyika, tunataka Lindi iwe mfano katika uongozi ndani ya UVCCM," anasema Matola.

Mwenyekiti huyo anasema umoja na mshikamano ndani ya jumuiya hiyo ni jambo la muhimu ambalo linaleta nguvu katika kuitumikia CCM na kwamba hivyo vyote vinapatikana kupitia madarasa hayo ya elimu ya uongozi.

Twaiba anafafanua kuwa mkoa huo una wilaya sita ikiwamo Liwale yenye kata 20, Nachingwea kata 36, Ruangwa kata 22, Kilwa kata 23, Lindi Mjini kata 31 na Lindi vijijini kata 20.

Anasema viongozi wa umoja huo wa ngazi ya kata watapaswa kuhudhuria madarasa ya elimu ya uongozi, kisha na wao wataishusha kwa viongozi wa ngazi ya matawi hadi mashina.

**AMEBAINI NINI?**

Mwenyekiti huyo anasema bado wapo baadhi ya viongozi wa jumuiya hiyo ambao hawajui wajibu wao, kitendo ambacho kama hawataingizwa katika madarasa ya elimu ya uongozi wanaweza kukwama kuongoza.

"Kwa mfano unakuta mwenyekiti anafanya kazi za katibu au katibu anafanya kazi za mwenyekiti, lakini wapo baadhi ya waliogombea uongozi hawajavunja makundi, hivyo ni vyema tuwekane sawa," anasema.

Anafafanua kuwa mwenyekiti ni msimamizi, katibu ni mtendaji, kila mmoja ana jukumu lake, hawapaswi kuingiliana, kwamba wapo wasiojua mipaka ya majukumu yao hadi wanafikia kuingiliana katika majukumu.

"Hayo na mengine mengi yanaweza kuisha iwapo watahudhuria katika madarasa ya elimu ya uongozi, nami nifuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kila kiongozi anahudhuria madarasa hayo," anasema.

Anasema suala la mafunzo katika uongozi ni la muhimu na kwamba ndio maana huwa kuna semina elekezi au madarasa ya elimu ya uongozi ni muhimu kwa manufaa ya jumuiya na chama kwa ujumla.

Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM kupitia Mkoa wa Lindi, Ramadhan Matola, anapigilia msumari kuwa ni lazima madarasa elimu ya uongozi yafanyike kwa viongozi wa kata zote kwa kila wilaya.

viongozi wa mkoa watatoa ushirikiano na ushauri ili jumuiya ya umoja wa Vijana Mkoa wa Lindi kuzidi kuimarika zaidi pia aliwapa taarifa kuwa madarasa mengine ya uongozi yatafanyika kwenye wilaya zingine kwa viongozi wa UVCCM wa kata zote kwa kila wilaya.

"Tutatoa ushirikiano na ushauri, ili Umoja wa Vijana Mkoa wa Lindi, uzidi kuimarika, ila madarasa mengi ya uongozi yatafanyika, tunataka Lindi iwe mfano katika uongozi ndani ya UVCCM," anasema Matola.

**SEMINA ELEKEZI**

Kabla ya kikao hicho kilichohudhuriwa na makada mbalimbali wa CCM akiwamo Katibu wa Chama wa Mkoa wa Lindi, Barnaba Essau, Katibu wa UVCCM wa mkoa huo, Pius Pukapuka na Mjumbe wa Baraka Kuu la UVCCM Taifa, Ramadhani Matola, linatolewa semina elekezi.

Semina inatolewa na Pukapuka ambaye anawataka viongozi wa umoja huo, ambaye anasisitiza kuzingatia kanuni za umoja huo na kutoingiliana katika majukumu yao ili kuimarisha UVCCM.

Katibu wa chama mkoa, Essau anasisitiza umuhimu wa viongozi hao kuzingatia majukumu yao kama yalivyoelekezwa kwenye kanuni ya UVCCM ili kutengeneza umoja imara ndani ya jumuiya.

"Kikubwa ni kuhakikisha Chama Cha Mapinduzi kinaendelea kuwa imara daima na pia nyie viongozi wa umoja wa vijana wafikieni vijana wengine walioko kwenye shule za msingi na sekondari ili kuongeza idadi ya vijana wa chipukizi na vijana wengine ndani ya UVCCM," anasema Essau.

Essau anasema ni jukumu la viongozi wa vijana kufuatilia hali ya kisiasa ya CCM na vyama vya upinzani kwenye maeneo yao, ili kuchukua hatua za kuimarisha CCM pale wanapoona kuna tatizo.

"Kumbukeni kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan ameruhusu mkutano ya hadhara, hivyo UVCCM ni jukum lenu kujibu hoja mara tu chama chetu kinapokosolewa," anasema.

# Congo inavyozidi kutumbukia kwenye balaa la mauaji, uasi

## •Mbele ya vikosi vya majeshi raia wachinjwa kama kuku

Na Gaudensia Mngumi

KINACHOENDELEA nchini DRC ni kitendawili, swali kubwa likibaki hivi itakuwaje mbona ni kama maji yameuzidi unga?

Kuna vikosi vya serikali pamoja na vya nchi majirani vilivyookaribishwa ili kuongeza nguvu ya kumaliza uasi na kuleta amani lakini raia wanauawa na kujeruhiwa mbele yao?

Ni hoja zinazoibuka kwasababu hali imezidi kuwa mbaya zaidi nchini DRC licha ya kusikika wadau mbalimbali wakipaza sauti kusaka amani akiwamo Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani Papa Francis, anayezuru Congo mwezi uliopita.

Lakini, Umoja wa Afrika (AU) nao ukitoa msimamo na kutaka mgogoro wa Congo sasa uwe historia, maagizo yanayotolewa karibuni baada ya mkutano wa wakuu wa nchi na viongozi wa serikali uliomalizika Addis Ababa, karibuni.

Mashambulizi na mauaji yamezidi licha ya Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kupeleka vikosi kukabiliana na machafu nchini Congo yanayochochewa na M23 na vikundi kadhaa vya waasi.

Wiki au mwezi Februari unamalizika kwa takriban raia 20 kuuliwa katika shambulizi linalofanywa eneo la kaskazini mashariki la linaripoti shirika la habari la Reuters

Linasema shambulio hilo lilitokea katika kijiji cha Kikura Jumapili jioni, taarifa zikitolewa na Odette Zawadi, Rais wa Shirika la Wanaharakati wa Kikura.

Anasema waasi wanashambulia kijiji hicho saa 9:00 usiku wakivamia raia na kuwapiga mapanga na kuchoma nyumba lawama zikielekezwa kwa ADF- Allied Democratic Forces.

Shambulio la hivi karibuni linakuja miezi kadhaa baada ya wanajeshi wa DRC na Uganda kuanzisha operesheni ya pamoja dhidi ya ADF, ambayo imeua maelfu ya raia katika eneo hilo tangu 2013.

Tangu operesheni hiyo ilipoanza mwishoni mwa Novemba mwaka jana, kundi hilo limeendelea kuwashambulia na kuwaua raia.

Desemba, takriban watu 16 waliuawa katika shambulio linalodaiwa lilifanywa na kundi la ADF katika maeneo ya vijijini huko Mangina.

### HAKUNA IMANI

Wakazi wa maeneo hayo wamekosa matumaini na imani na shughuli zinazoelezwa kuwa zinafanywa na vikosi vya pamoja vya EAC, wakihoji unawezaje kueleza kuwa watu 20 wanauawa mbele ya vikosi hivi viwili? Zawadi analiambia Shirika la Reuters

Katika shambulio hilo miili 20 ilibainika kwenye mauaji yanayofanyika wakati wananchi walifikiria kuwa vikosi vya muungano wa majeshi ya Kongo na Uganda vingesaidia, lakini wamebaki vinywa wazi na kuzidi kusikitika.



Ndivyo Congo ilivyojaa waasi, majeshi na silaha. **PICHA: THE DEFENSE POST**

Wakati vilio vinakolea Mashariki mwa DRC kwenye mapambano na M23, mashambulio kutoka kwa vikosi vya ADF iliyoanzishwa nchini Uganda mwaka 1995 nayo yanaanza kukolea sehemu nyingine za nchi hiyo.

Baada ya kuundwa Uganda ADF ilihamia DRC na sasa ni miongoni mwa makundi mengi yenye silaha yanayotafuta udhibiti wa maeneo na rasilimali za hasa madini mashariki mwa nchi hiyo.

Awali kulikuwa na madai kuwa ina ukaribu na kundi la Kiislamu la ISIL au ISIS taarifa zilizoibuka 2019, hata hivyo watafiti wa Umoja wa Mataifa (UN) wanaeleza kuwa hawajapata ushahidi wowote kwamba kikundi hicho cha ISIS kina udhibiti wa ADF.

### TAMBO ZA VIKOSI

Vikosi vya Uganda vimekuwa vikieleza kuwa vimeanzisha mashambulizi ya anga na mizinga nchini DRC tangu kuanza kwa operesheni hiyo ya pamoja na kuahidi kuendeleza harakati za kutokomeza uasi katika nchi hiyo jirani kwa muda mrefu iwezekanavyo ili kuwadhibiti na kuwafurumusha ADF.

Msemaji wa Jeshi la DRC, Antony Mwalushayi, anaiambia Reuters kwamba wanajeshi katika eneo hilo wanachelewa kujua kuhusu shambulio la hivi karibuni kwa sababu wavamizi hawakutumia silaha badala yake walikwenda na mapanga, marungu na kuchoma moto.

Anaeleza kuwa kubadilisha mbinu za kivita ni tatizo na kwamba hawatakata tamaa, licha ya kuwapo kwa matukio hayo.

"Hatuwezi kuvunjika moyo kwa sababu lengo la adui ni kutuvunja moyo, kutugombanisha na kutuvurugia uhusiano wetu na watu," anasema Mwalushayi.

### HALI MBAYA

Mwezi uliopita Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Ilze Brands Kehris, alizuru DRC ikitembelea mji mkuu wa Kinshasa na miji ya mashariki ya Goma na Bunia na kueleza hali ya wasiwasi anayokutana nayo.

Ilze anaelezea kusikitishwa na kuzorota kwa hali ya usalama mashariki mwa nchi, ambapo mamia ya vikosi vya kiasi kuanzia M23, ADF na CODECO vinavyoendelea na harakati za kuua raia.

Miongoni mwa taarifa za ukiukaji na ukiukwaji wa haki za binadamu zilizorekodiwa DRC ni pamoja na mauaji ya watu wengi, kukata watu mapanga, unyanyasaji wa kingono, mateso kwa raia, kuongeza kiwewe na kusababisha watu wengi kuhama makazi yao na kuwa wakimbizi wa ndani na nje ya mipaka.

"Ninalaani vikali mashambulio ya kutisha katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na naungana na Katibu Mkuu wa UN anayetoa wito wa kuwapo 'hatua kwa ajili ya amani ya Afrika'".

Anasema vurugu lazima zikome. Pia anahimiza sana wadau kuanzia vikosi vya EAC na mamlaka nyingine kuzidisha juhudi za kukabiliana na uhasama na chuki inayoongezeka nchini Congo, akizitaka pande zinazohusika kutekeleza mipango inayolengwa ili kukuza na kuongeza mshikamano wa ndani na kati ya jamii inayolizunguka taifa hilo.



AFP

JUKWAA LA UONGOZI

SHAMIM KHAN

# Mbunge, waziri aliyeacha nyayo kuinua wanawake kwenye uchumi na biashara

## •Mwasisi wa mabanda ya kinamama Sabasaba

**Na Christina Mwakangale**

KATI ya wanawake wanasiasa walioshika nyadhifa mbalimbali za uongozi serikalini, jina la Shamim Khan limo kwenye orodha.

Anaanza na uwakilishi, tangu mwaka 1985 hadi 1995 anawawakilisha wapigakura wa Jimbo la Morogoro Mjini, wakati wa awamu ya pili.

Kadhalika, mwaka 1995 hadi 2005, anakuwa mbunge viti maalumu, wakati huo Rais Benjamin Mkapa akishika usukani, anamteua kuwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara mwaka 1995.

Shamim, anasema kitaaluma ni mwalimu, mambo anayoyaeleza kwenye mahojiano na Nipashe hivi karibuni. Anazungumzia safari ya maisha yake kisiasa akisema alipoamua kuchukua fomu na kugombea nafasi ya ubunge Morogoro Mjini, anatimizi kiu ya kuwa kiongozi.

Anasema ni baada ya kutamani kuwa mwanasiasa na kiongozi wa wananchi mwenye kuja na ajenda za wanawake, kuzipigania na kuzitetea.

"Zamani nako masuala ya usawa wa kijinsia yalikuwapo na kuna wakati wanawake wachache walijitokeza kugombea uongozi. Siku naenda kuchukua fomu, nikakuta wanaotoa fomu wote ni wanaume. Wakasema nawe unagombea." Anakumbuka.

Anaongeza kuwa walimu wakati huo ndiyo walitegemewa sana kwenye sekta nyingi za umma akitoa mfano kuwa walichukuliwa kusimamia na kuhesabu kura.

"Nilitamani kugombea, nikisema kwa nini kila uchaguzi nimhesabie kura mwingine tena ni mwanaume? Nami naweza. Mfumo dume ulitamalaki katika siasa, nikaenda kuchukua fomu na nikapitishwa kugombea," anasema.

Mwalimu Shamim anaeleza kuwa mwaka 1984 mwishoni, aliyekuwa mbunge wa Morogoro Mjini, anatangaza kuachia uongozi naye akapata fursa akaingia kwenye uchaguzi kwa sababu kiti chake kilikuwa hakina mtu.

"Nilipofika nyumbani nikamweleza mume wangu akasema unaweza kuingia na cha ajabu nilipata mchango mkubwa wa familia yangu kwa ukubwa mno na wakati huo mzee, baba yangu Khan alikuwa hai."

"Nilikwenda kuchukua fomu na siku ya mwisho, ajabu lakini nikakuta wamekaa wanaume na wakaniita Mwalimu Khan, vipi umekuja kuchakua fomu? Wakanipa fomu ya Viti Maalumu. Nikasema nataka fomu ya kuwa mbunge nipambane mwenyewe wakati huo walitaka apite mwanaume kama unavyojua wanawake hatuaminiki kila sekta," anaeleza Shamim.

Anasema ulipofika wakati wa mkutano na wagombea wakiwa zaidi ya 30 na kuchujwa, kwenye mchujo akawa wa pili wa kwanza alikuwa mwanaume na kwamba majina yalipopelekwa CCM Makao Makuu, likarudisha jina lake.



Shamim Khan, akizungumza kwenye kongamano la kuadhimisha miaka 15 ya Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T), Dar es Salaam. **PICHA: MWANDISHI WETU**

**NI BEIJING, DAR**

Shamim, anakumbuka miaka ya 1990 wakati wa vuguvugu la mapinduzi ya uongozi wa wanawake duniani, ukiwamo pia Mkutano wa Dunia wa Wanawake wa Beijing, akisema lilisaidia kujenga ujasiri kwa mwanamama anayetarajia kuwa kiongozi.

"Mheshimiwa Mkapa akawapokea waliotoka Beijing kina Mama Getrude Mongela. Nakumbuka magazeti yaliandika 'Beijing comes home'. Sasa mimi kama Naibu Waziri wa Viwanda mwanamke tutawasaidiaje wanawake wenzetu kufikia malengo yao ya biashara? Nikawaita wafanyakazi wa Wizara ya Viwanda na Biashara, akiwamo Naibu Katibu Mkuu wangu Hanifa Mohamed Karamagi."

Anasema wakaazimia kuwa wao ni wanawake lazima wafanye jambo zuri kuwasaidia wanawake wakawa na wazo kwenye Maonyesho ya Biashara Sabasaba wakapanga kuanzisha vibanda vya biashara vya wanawake.

Anaeleza kuwa mwanamke anapopata fursa ya kuongoza wengine, kuwapo kwa ajenda maalum za kuikwamua jamii husan mwanamama ni muhimu na kwamba hadi sasa alama yake ipo, akiwa mtoa wazo la wanawake kushiriki maonyesho ya biashara Sabasaba.

Anaongeza kuwa akiwa Naibu Waziri, mara kadhaa anafika kwenye mikoa mbalimbali na kuwaona kinamama na bidhaa zao tofauti, mfano vijijini anakuta wanawake wengi wana bidhaa nzuri na bora, wengine hawajui hata kupanga bei zake.

Anakumbusha kuwa wanunuzi wao walikuwa wenye magari na kwamba mpaka magari yawafikie kununua lakini hata bei yao haikuwa nzuri ni ile waliyoitaka, siyo yenye tija kwa wazalishaji.

**KUUNGANISHA WANAWAKE**

Shamim anasema alipata wazo la kuwakusanya wanawake hao kutoka mikoa kadhaa ikiwamo visiwa vya Zanzibar na kuanza kuwaleta pamoja kwenye mikutano na matamasha, kisha kuwaunganisha na maofisa wa umma.

"Tukaanza kuhangaikia namna ya kuwaleta wanawake kwenye biashara tukaongea na maofisa biashara wa mikoa mbalimbali wawalete na pia tukawatumia mofisa wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Watoto.

"Maofisa hao wanajua wanawake wa maeneo gani, wawalete wanne kwa kila mkoa na pia tukawaambia wajitegemee kila kitu kwa sababu ni mara ya kwanza."

Anasema hakukuwa na chochote kuwawezesha, wengine walilala hotelini kwa wenye uwezo kiasi, walilala kwenye mabanda Sabasaba kulikokuwa na usalama na ulinzi.

Anawapongeza kinamama kuwa hawakukata tamaa licha ya wanawake wengine kutoka Zanzibar na mikoa mbali zaidi.

Anasema zilikuwa bidhaa zilizoletwa kutoka mikoa tofauti, nyingine zilikuwa na hali mbaya na baadhi zilikuwa bora.

"Changamoto nyingine wengi wao hawakujua kupangilia bei mfano kuna mama alileta jamvi dogo akasema nauza 200,000 nikakaa naye na kumuuliza ulitumia muda gani kutengeneza, alipata wapi ukindu? Kwa ujumla hawakuwa na maarifa ya namna ya kupanga bei," anasema Shamim.

Anasema mwaka uliofuata, walioteuliwa katika mikoa yao waliitwa mapema wakishirikiana na Mama Anna Mkapa akiwa na Taasisi ya Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) walitafuta wafadhili, ili kutoa mafunzo ya uwezeshaji mbinu za kujikwamua na kuinuka kibiashara kwa wanawake hao.

Baada ya mafunzo, Shamim anasema aliyaona mabadiliko ingawa vilikuwapo vikwazo kadhaa kama kinamama hao kutakiwa kulipia fedha kwa wadhibiti ubora na viwango TBS, huku wakilalamika kuwa bado hawajainuka.

"Namshukuru sana Mama Mkapa tukaanza semina ya siku tatu, tunawaelimisha namna ya kupanga bidhaa bora. Nikapata taarifa kwa baadhi ya wafanyabiashara wanawake hao, kuwa wanapokwenda TBS wanaambiwa walipe pesa na hawana hela."

"Nikaongea na TBS nikawaambia kwa sababu hawa kinamama wanaanza tuwape muda kidogo hakuna haja ya kuwalipisha na tukaafikiana hivyo." Anaeleza.

Anasema mabadiliko yakaja, wakaanza kupata soko la ndani na nje, huku wajasiriamali wa madini wakitambulika nje pia na kwamba waliwaambia watengeneze bidhaa ndogo ndogo, ili mtu wa nje akija aondoke na bidhaa nyingi akawauzie wengine.

"Nakumbuka nilikwenda kijiji fulani nikakuta pale kijijini kuna mashine za kusaga na kukoboa tano na ni nzuri lakini hakuna wateja hadi mashine ya tano nikakuta watu wamejaa mno na kugundua yule mfanyabiashara alikuwa mbunifu, aliweka televisheni kuwavutia watu."

Kadhalika alikutana na wafanyabiashara wa viazi waliokuwa wanauza bila viroba, akawapa elimu kuwa wanunue viroba wawauzie wateja na watapata pesa zaidi.

"Baadhi ya viazi havikoshwi inabidi uwaambie wavioshe na walikuwa wanaosha tulikwenda hatua kwa hatua na sasa tumefanikiwa," anasema Shamim na kuongeza;

"Tumetokea mbali nashukuru tumeacha alama kubwa huko nyuma. Kila nikienda Sabasaba najisikia na kusema kwamba hapa kuna mkono wangu," anaeleza.



# TaCRI yaweka mikakati kuondoa uhaba wa miche ya kahawa

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI) imeweka mikakati ya kuziba uhaba wa mahitaji na upatikanaji wa miche ya zao hilo miongoni mwa wakulima wa ndani.

Mahitaji ya miche ya kahawa nchini kwa sasa ni kati ya milioni 50 hadi 60 kwa mwaka, lakini uwezo wa TaCRI ni kuzalisha miche milioni 20 kwa mwaka.

Akiongea wakati wa mahojiano maalumu na Nipashe Mkurugenzi Mtendaji wa TaCRI, Dk. Deusdedit Kilambo, alisema upungufu huo unawafanya wakulima wengi wa kahawa wasifikie uwezo wao kamili wa uzalishaji.

"Tumedhamiria sana kuzalisha miche ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya wakulima katika mikoa yote ambayo zao hilo linastawi, lakini kwa bahati mbaya kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukishindwa kuzalisha miche mingi kutokana na sababu mbalimbali zilizo nje ya uwezo wetu," alisema.

Sambamba na hilo alisema taasisi hiyo yenye makao yake makuu mkoani Moshi hadi sasa imefanya utafiti na uzalishaji wa aina zisizopungua 19 ya kahawa aina ya arabika pamoja na aina nne za robusta.

Aidha, alifafanua zaidi kwamba aina hizo zina uwezo wa kutoa kati ya tani mbili hadi sita kwa hekta moja ya kahawa safi (maharage ya kijani kibichi).

Alisema kuwa kahawa ya Tanzania haikabiliwi na changamoto yoyote bora katika soko la dunia kwa sababu aina inayozalishwa na TaCRI ni miongoni mwa aina bora zaidi duniani.

# Dira za maji zatajwa suluhisho wananchi kubambikiwa bili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MATUMIZI ya dira za maji za malipo ya kabla zimetajwa kuwa suluhisho la malalamiko ya wananchi kubambikiwa ankara na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira nchini.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA), Mhandisi David Palangyo, alibainisha hayo jana jijini hapo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mamlaka hiyo.

Alisema hadi sasa mamlaka hiyo imefunga dira za malipo ya maji kabla kwa wateja na taasisi mbalimbali zaidi ya 6,700 ambazo zimesaidia kupunguza malalamiko kwa wateja.

"Toka kuanza kufunga mita hizi za maji mwaka 2015 kumekuwa na mafanikio makubwa sana tumefanikiwa kupunguza malalamiko ya wateja kubambikiziwa ankara za malipo ya maji pia tumepunguza malimbikizo ya madeni kwa wateja wetu wakiwamo wadaiwa sugu,"alisema.

Aidha, alisema hadi sasa mamlaka hiyo inadai zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa wateja wadogo ikiwa ni sehemu ya deni lililokuwapo kabla ya kufungwa kwa dira za malipo ya maji kabla.

"Taasisi zote za serikali tumewafungia dira hizi hivyo kusaidia kuondokana na changamoto za kudai madeni ya malipo ya ankara kama ambavyo maeneo mengine wamekuwa na changamoto hizo,"alisema Palangyo.

Kadhalika, alisema lengo la mamlaka hiyo ni kuwafungia dira hizo wateja wote ambao wanatumia huduma ya mamlaka hiyo ili kupunguza malalamiko na kuongeza mapato.

Vile vile, alisema hadi sasa huduma ya maji safi katika Mkoa wa Iringa imewafikia wananchi kwa zaidi ya asilimia 97 na mikakati ya kuwafikia wananchi wote inaendelea.

"Tunaishukuru sana serikali yetu kwa kutupatia fedha ambapo hivi sasa tunatekeleza miradi ya maji inayogharimu zaidi ya Sh. bilioni 220,"alisema.

Alisema pamoja na mafanikio hayo mamlaka hiyo bado inakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo uharibifu wa mazingira unaosababisha ukame na kupungua kina cha maji.

Hata hivyo alisema mamlaka hiyo inaendelea ni jitihada mbalimbali za kuongeza huduma ya uondoshaji majitaka ambapo hivi sasa imewafikia watu kwa asilimia 6.8.



Makamu Mwenyekiti wa soko la Sabasaba, Kombo Adamu Kombo, akizungumza na wafanyabiashara jijini Dodoma jana wakati akitoa taarifa kuhusu hatima yao ya kuondolewa na Halmashauri ya Jiji hilo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waislamu wapewa angalizo uwapo wa taasisi za kitapeli

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, amewaonya viongozi wa dini ya kiislamu kujiepusha na taasisi za kitapeli za mfukoni ambazo hazitambuliwi na serikali wala Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA).

Alitoa tahadhari hiyo wakati akizungumza na viongozi wa BAKWATA Wilaya ya Dodoma kwenye mkutano mkuu.

Aliwataka kujiepusha na uanzishaji wa taasisi ambazo hazitambuliwi na serikali, BAKWATA hata na jamii inayowazunguka.

Alisema kuwa BAKWATA Mkoa wa Dodoma haliko tayari kuwafumbia macho wale wote watakaojihusisha kuwa na taasisi za mfukoni za kitapeli.

Alisema kuwa taasisi hizo hazitafumbiwa macho kwa sababu zimekuwa zikiwanufaisha wao wenyewe bila kutambua kuwa kwa kufanya hivyo pia ni dhambi kutokana na kutowafikia walengwa.

"BAKWATA kamwe haitakubali kuona wezi hao wanaoibia serikali kupata kodi yake wakiachwa kupiga hela, huku wakijifanya ni waumini wazuri wakati ni matapeli," alisema.

Akizungumza na viongozi hao kutoka ngazi ya mashekhe, maimamu na walimu, pia aliwataka kujitambua kwenye nafasi zao ili waweze kuitumikia BAKWATA.

Alisema kuwa bado kuna kero kwa baadhi ya viongozi wa BAKWATA ambao wana taasisi lakini hazijasajiliwa na kutambuliwa na serikali, akisema kazi yao kujimilikisha mali kwa faida yao.

Shekhe Rajabu aliwataka viongozi hao wa BAKWATA wilaya ambao hawajitambui kwenye nafasi zao wabadilike na waache kufanya kazi kwa mazoea vinginevyo wajiondoe kwenye nafasi za uongozi.

"Bado kuna tatizo miongoni mwa viongozi wa BAKWATA hawajiamini kwenye nafasi zao na walio wengi wanafanya kazi kwa mazoea na kushindwa kubadilika hapa niwatake sasa mbadilike na mwondokane na tabia ya mazoea ambayo hayana tija ndani ya uisilamu," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania Wilaya ya Dodoma, Bashiru Hussen, amewataka viongozi kuwa wabunifu katika utendaji wao wa kazi ili waweze kusaidia uislamu na kwa waumini wao wanaowaongoza.

Alisema baadhi ya viongozi hawana mabadiliko kwenye nafasi zao hali ambayo imekuwa ikiudumaza uislamu na waumini wao.

Pia aliwataka viongozi kuendelea kudumisha amani na umoja huku wakifanya kazi kwa kushirikiana na kukemea maovu yote yanayojitokeza.

Alisema: "Nyinyi ndiyo mabalozi wetu kwa waumini ambao mnaowaongoza huko kwenye misikiti yenu, hivyo niwatake sasa mkajisimamie wenyewe katika nafasi za kushirikiana kupendana kudumisha amani na umoja na sivyo vinginevyo."





# Wakulima wa tumbaku walia ucheleweshaji wa mbolea

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKULIMA wa tumbaku Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya (CHUTCU) wameishauri serikali kufanya maandalizi mapema ya upatikanaji wa mbolea zinatotumika kwenye zao hilo.

Wamesema kufanyika kwa maandalizi hayo mapema kutasaidia kuondokana na tatizo la kuchelewa kwa mbolea hizo ambazo zimekuwa ikiwasababishia hasara wakulima kwa kupata mavuno kidogo.

Walitoa ushauri huo juzi kwenye mkutano mkuu wa 23 wa tumbaku wilayani humo na kueleza kuwa ucheleweshaji wa mbolea unaweza kusababisha upatikanaji wa tumbaku isiyokuwa na ubora.

Hivyo waliiomba serikali kuingilia kati madeni yao wanayodai kwa wanunuzi wa tumbaku.

Mmoja wa wakulima hao, Anna Jeremiah, alisema katika msimu huu wakulima wamepanda mbegu tangu Desemba mwaka jana na kwamba mpaka sasa hawajapata mbolea hali ambayo inawapa hofu ya kupata mavuno hafifu.

"Tunakabiliwa na tatizo la kuchelewa kwa pembejeo hasa mbolea na lingine ni kushuka kwa mahitaji ya tumbaku hivyo kusababisha kampuni nyingi kujitokeza kununua tumbaku ambayo yalikua siyo ya uhakika yamepelekea vyama kutolipwa fedha hadi sasa," alisema Anna.

Mkulima mwingine, Richard Kilongozi, alisema ili zao hilo listawi vizuri linapaswa kuwekewa mbolea kwa wakati na kwamba kwa msimu huu wa kilimo wamepanda zao hilo kwa wakati lakini kuchelewa kufika kwa mbolea kutasababisha washindwe kuvuna mazao bora.

"Kwa kweli mbolea zimeanza kufika lakini hazijafika kwa wakati muafaka na saizi kuna tatizo kubwa juu ya mbolea ya CAN na UREA, tumepanda kwa muda muafaka lakini mpaka sasa zao hili halijapata virutubisho vya mbolea na hiyo sasa itasababisha zao hilo kutokua na ubora hali itakayosababisha soko liwe chini ya kiwango," alisema Kilongozi.

Mrajisi Msaidizi Mkoa wa Mbeya, Rechard Zengo, aliwataka wakulima kushirikiana na chama kinachowasimamia ili kudai madeni hayo huku akiagiza vyama vya ushirika kusikiliza kero za wakulima na kuzitafutia ufumbuzi kwa wakati.

Mwenyekiti wa mradi wa pamoja wa Vyama Vikuu vya Tumbaku(TSJE) , John Ntenzilyo, alisema watahakikisha wanapitia mikataba yote baina ya kampuni za ununuzi wa tumbaku na wakulima ili kuhakikisha wakulima wanalipwa madeni yote na kutatua tatizo la mbolea.

"Ni kweli kumekuwa na tatizo la ucheleweshaji wa mbolea na hii ni kutokana na mahitaji makubwa ya mbolea hii na sio Chunya tu hata maeneo mengine wanakolima zao hili kumetokea tatizo hili lakini maelekezo ya serikali ni kuhakikisha vikwazo hivyo vinatatuliwa na mbolea zinawafikia wakulima kwa wakati," alisema Ntenzilyo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Mbeya jana, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yanayotarajiwa kufanyika kimkoa wilayani Rungwe Machi 8, mwaka huu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanaopinga ukatili waomba ushirikiano ngazi ya familia

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WADAU wa masuala ya ukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Mbeya wameomba ushirikiano kuanzia ngazi ya familia ili kukabiliana na vitendo vya ukatili.

Akizungumza juzi na Nipashe, Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Mbeya, Loveness Mtemi, alisema kuwa lengo la mpango huo ni kutokomeza vitendo hivyo ambavyo ni vya ubakaji, ulawiti na vipigo.

Alisema licha ya wanawake na watoto kuwa waathirika wa matukio hayo kuna tatizo la watu hao kutotoa taarifa wanapofanyiwa vitendo vya kikatili.

"Kuna tatizo kubwa la vitendo vya ukatili wa kingono kwa wanawake na watoto mbaya zaidi hawatoi ushirikiano kwa Jeshi la Polisi wanawakumbatia watuhumiwa kutokana na mahusiano waliyonayo kwenye familia zao naomba tubadilike," alisema Mtemi.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Anna Gereta, alisema hospitali hiyo imekuwa ikipokea watoto wengi ambao wanafanyiwa vitendo vya kikatili. Alisema miongoni mwa vitendo vinavyoripotiwa ni ulawiti kwa watoto wakiume na wakike na kwamba wanapohitaji ushirikiano kutoka kwa wazazi wanakosa.

Alisema licha ya hospitali hiyo kupokea watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili, alidai mpango mkakati huo waliokubaliana katika kikao hicho utaleta tija kwani wataendelea kutoa elimu kwa kuwashirikisha wazazi na walezi.

Alisema kuwa wanaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa wananchi ili kujenga uelewa wa namna ya kuepukana na vitendo hivyo.

## M/kiti CCM akemea chuki, visasi na majungu kwa wanachama

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, Dk. Steven Mwakajumilo, amewataka wanachama wa chama hicho kuachana na chuki, visasi na majungu ambayo yanasababisha migogoro na kutoa nafasi kwa vyama vya upinzani kuwasema kwenye majukwaa ya kisiasa.

Alitoa kauli hiyo wilayani Kyela alipozungumza na wanachama wa chama hicho kuhusu uzalendo.

"Mbeya tunapakana matope sana, Mbeya tuna chuki mno, ni wachache sana wanaowasemea mazuri wenzao, huwa tunazuia ridhiki ya mtu mwingine kwa sababu ya chuki, niwasihii tubadilike tuwe wamoja tuache maneno tutimize wajibu wetu, anapatajwa mwenzio kwa mazuri muunge mkono na kama kuna matatizo mshauri na mwonyeshe njia, alisema Dk. Mwakajumilo.

Alisema wasomi pamoja na vijana wengi mkoani Mbeya, wanatumia mitandao ya kijamii kama fimbo ya kuwapigia wengine badala ya kuelimisha jamii.

Hivyo aliwataka Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) kuepukana na makundi hayo na badala yake watumie nafasi hiyo kusahihisha makosa na kutafuta fursa mbalimbali za kimaendeleo.

Aliwaagiza madiwani wote kuhakikisha wanasoma Ilani ya chama hicho wanapokutana na wananchi wao katika mikutano na miradi inayotekelezwa katika maeneo yao, huku akiwataka viongozi kutumia lugha za staha wanapokuwa katika majukwaa.

"Miradi mingi inayotekelezwa wananchi hawajui hivyo tuwaeleze na viongozi mnapofanya ziara tembeleeni makundi mbalimbali ongeeni nao mtajua changamoto zao ili uwe na uhakika na unachojibu, lakini hata kama serikali italeta fedha kama hakuna maelewano miradi itakwama kutekelezwa niwaombe tuondokane na migogoro,"alisema Dk. Mwakajumilo.

Katibu wa UVCCM Mkoa wa Mbeya, Yusuph Mabena, alisema mbio hizo za bendera ya miaka 46 ya CCM zitakimbizwa wilaya zote saba za Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kupeleka ujumbe kwa wanachama, kuyavunja makundi, kuimarisha umoja na mshikamano, kubuni miradi ya kimaendeleo na kuongeza wanachama wapya.



# Serikali kuimarisha mabonde sita kujitosheleza na chakula

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakusudia kutekeleza mpango mkuu wa kujitosheleza kwa chakula kwa kuimarisha mabonde sita yenye hekta 1,053.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Ali Ameir, aliyetaka kujua mipango ya wizara ya kujitosheleza kwa chakula katika kilimo cha umwagiliaji umefikia hatua gani.

Aliyataja mabonde hayo ni Cheju lenye ukubwa wa hekta 314 ambalo limekamilika kwa asilimia mia katika ujenzi wa miundombinu yake.

Aidha, alilitaja bonde lingine la Kinyasini lenye ukubwa wa hekta 184 ambapo ujenzi wa miundombinu yake ya kupitisha maji umekamilika na tayari wakulima wameanza kulitumia kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo cha umwagiliaji maji cha mpunga.

Alisema zaidi ya wakulima 2,500 wamepatiwa maeneo hayo tayari kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani baada ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu yake.

''Mheshimiwa Naibu Spika niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba mchakato wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika mabonde ya mpunga umekamilika na wakulima tayari wameanza shughuli za kilimo huku matarajio ya wizara ni kupatikana kwa mafanikio makubwa,''alisema.

Akifafanua zaidi alisema kazi kubwa inayofanywa na maofisa wa kilimo ikiwamo mabibi shamba na mabwana shamba ni kutoa elimu pamoja na kuwafikia wakulima wa mpunga kwa kuwapatia mbinu bora za kulima kwa mafanikio makubwa.

Alizitaja changamoto zinazowakabili wakulima wa kilimo cha mpunga ni kulima kwa mazoea na kushindwa kutumia utaalamu ikiwamo mbolea kwa ajili ya kupata kipato kikubwa.

Alisema: ''Hizo ndiyo changamoto zinazowakabili wakulima wa mpunga Unguja na Pemba kiasi cha kushindwa kuyafikia malengo ikiwamo kulima mpunga na kuuza kibiashara...bado wanatumia mbinu zilizopitwa na wakati zinazotokana na urithi wa wazazi wao''.

# SMZ yatoa ufafanuzi ucheleweshaji majibu Hospitali ya Mnazi Mmoja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema uchelewaji wa upatikanaji wa majibu ya vipimo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kutokana na aina ya kipimo husika na mchakato wake, kwamba baadhi ya vipimo huchukua zaidi ya saa tatu.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Viti Maalum, Salma Mussa Bilali, aliyetaka kufahamu utatuzi wa changamoto ya vifaa tiba katika hospitali hiyo.

Alisema miongoni mwa vifaa hivyo ni kipimo cha Blood Culture ambacho ni cha tezi dume mchakato wake unachukua siku saba ili kupata majibu.

"Napenda niwajulishe wajumbe kwamba kuchelewa kwa majibu ya vipimo kunasababishwa na aina ya kipimo na utaratibu wa kuchakata vipimo ili kutoa majibu," alisema Naibu Waziri huyo.

Aidha, alisema ili kuhakikisha upatikanaji wa vifaa tiba vya kisasa na vitendanishi vyake kwa lengo la kuboresha huduma za uchunguzi, Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya imeamua kuwapa wakala huduma za uchunguzi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Alisema miongoni mwa vifaa hivyo, huduma za maabara kwa 'lancet' na rediolojia kwa NSK, lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa vipimo kulingana na mahitaji halisi ya wananchi.

Naibu waziri huyo alisema katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za uchunguzi kwa wakati, Wizara ya Afya imefikia maamuzi ya kutoa huduma za uchunguzi kupitia wakala.

Alisema tayari taratibu za kufunga mkataba wa makabidhiano zimekamilika kuanzia Febuari 1 mwaka huu na huduma za rediolojia zimeanza kutolewa.

Hata hivyo alisema juhudi zinachukuliwa kukamilisha taratibu za makabidhiano na 'lancet' kwa ajili ya kuanza kutoa huduma za maabara.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Gulamu, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara ya Elimu yakiri upungufu wa walimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imesema suala la upungufu wa walimu kwa shule nyingi ni changamoto kwa wizara hiyo.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Gullam, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mtabwe, Habib Ali Muhammed.

Mwakilishi huyo alihoji tatizo hilo la uhaba wa walimu hasa kwa Shule ya Makongeni Mtambwe Pemba ambayo ina walimu wawili wanaolazimika kufundisha madarasa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Akitolea ufafanuzi wa hoja hiyo, alisema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar inaendelea kulifanyia kazi suala hilo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

Alisema kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara inategemea kuajiri walimu 1,328 kati ya hao walimu 250 ni wa sekondari, 590 msingi na 488 maandalizi.

Aidha, alisema walimu hao watapelekwa katika shule zenye mahitaji makubwa visiwani Unguja na Pemba.

Alisema wizara tayari imeshapeleka walimu wawili katika Shule ya Makongeni kupunguza changamoto ya walimu katika shule hiyo.

Hata hivyo alisema wizara pia inategemea kuongeza walimu katika shule hiyo baada ya kupatikana kwa walimu katika mchakato wa ajira unaoendelea.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO LA KUHAMISHA UMILIKI WA KIWANJA

Taarifa inatolewa kwamba **MARY ANITA NGOWI** mmiliki aliyeandikishwa **KIWANJA NA. 17 KITALU '11' KIBADA** anakusudia kuhamisha umiliki wa eneo hilo kwenda kwa **WALTER CLINT TENGA** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda siku 30 tangu tarehe ya taarifa hii.

P.A. Masoy
AFISA ARDHI MTEULE
MANISPAA YA TEMEKE

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED THE REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF KIGOMA)**
**AT KIGOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FR.MSGR LIBERATUS NYAMGUMA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF PROBATE**
**BY**
**FR. FRANK JOHN GILAGIZA.......PETITIONER**

### GENERAL CITATION

All person claiming to have any interest in the estate of the above –named deceased who died intestate, are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of the probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 09th day of March, 2023.
The Will of the deceased, (if any), is deposited and open for inspection at the court.
Dated at KIGOMA this 13th day of February, 2023.

DEPUTY REGISTRAR
.........................................
**DEPUTY REGISTRY**

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED THE REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE SUB REGISTRY OF KIGOMA)**
**AT KIGOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FR. EZEKIEL BUTHOKE**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF PROBATE**
**BY**
**FR. FRANK JOHN GILAGIZA.........PETITIONER**

### GENERAL CITATION

All person claiming to have any interest in the estate of the above –named deceased who died intestate, are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of the probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 09th day of March, 2023.
The Will of the deceased, (if any), is deposited and open for inspection at the court.
Dated at KIGOMA this 13th day of February, 2023.

DEPUTY REGISTRAR
.........................................
**DEPUTY REGISTRY**

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED THE REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF KIGOMA)**
**AT KIGOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FR.VEDASTUS NYAMURUNDWA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF PROBATE**
**BY**
**FR. FRANK JOHN GILAGIZA.........PETITIONER**

### GENERAL CITATION

All person claiming to have any interest in the estate of the above –named deceased who died intestate, are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of the probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 09th day of March, 2023.
The Will of the deceased, (if any), is deposited and open for inspection at the court.
Dated at KIGOMA this 13th day of February, 2023.

DEPUTY REGISTRAR
.........................................
**DEPUTY REGISTRY**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**GASPAR DAMAS MASHINGIA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0175/0511** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SALESIANS OF DON BOSCO-DODOM**A mwaka 1994 na cheti cha kidato cha nne chenye majina **GASPER DAMAS MASHINGIA** chenye index namba: **S0165/0013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia URU SEMINARY SCHOOL mwaka 1991. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/74655/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**MAHAKAMA YA TANZANIA.**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Korogwe, Kituo cha Manundu, Mkoa wa Tanga.**
**Shauri la madai Na. 11 /2023.**

**Jina la mdai:................................... Kelvin Deus Buriti**
**Jina la mdaiwa:......................... Hossein Said Mkufya.**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

**Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu madai katika Mahakama ya Mwanzo kwa Afisa Mtendaji Habitati**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya pesa sh. 3,500,000, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii 1/3/2023 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili, ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**Angalizo:** kama hautohudhuria siku uliyotajwa hapo juu, na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MANUNDU - KOROGWE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MPWAPWA**
**Kituo cha MPWAPWA MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai /Ndoa Na 5 ......................2023**
**Jina la Mdai MONICA % MWACHA**
**Jina la Mdaiwa JORAM % MBEDEGARO**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa JORAM %MBEDEGARO .......... MKAZI WA KOTA MPWAPWA MJINI**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba (Eleza hapa habari za Madai) MDAIWA ANADAIWA NA MDAI MAGUNIA 320 YA ALIZETI YENYE THAMANI YA TSHS 20,280,000/**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 13 Mwezi 3 Mwaka 2023 Saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28 Mwezi 2 Mwaka 2023

...............

---

**MWAMBA MILLENIUM COMPANY LIMITED**
**CHIMWAGA DODOMA**
**MNADA WA HADHARA**
**SHAURI LA NDOA NO. 10/2022**

KWA AMRI YA MAHAKAMA YA MWANZO MAKOLE WILAYA YA DODOMA MJINI TUTAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA NYUMBA ILIYOPO KISASA KIWANJA NO.43 KITALU L, NA KIWANJA NO 32 KITALU O KILICHOPO NKUHUNGU MALI YA WANANDOA, MARIAM GAU NA ABDULKARIM NDWATA NDANI YA SIKU 30 MGAWANYO WA TALAKA.MNADA UTAFANYIKA TAREHE 30/3/2023 SIKU YA ALHAMISI SAA TANO KAMILI ASUBUHI (05:00) NA SAA SABA KAMILI (7:00) HUU MNADA UTAFANYIKA KISASA NA NKUHUNGU

**MASHARTI YA MNADA: -**

- UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.
- MALIPO 25% BEI ITAYOWEKWA KWENYE MNADA NA 75% ATAMALIZIA NDANI YA SIKU 14
- ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOWEKWA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE.
- KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA KWA SIMU NAMBA **0712245977, 0784155866,0684364501,0767245977**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

---

**LAND DISPUTE COURTS (THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL)**
**GN NO. 174**
**FORM NO. 28**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA TUNDURU**
**MAHALI: TUNDURU**
**MAOMBI NO. 13/2022**
**OMARI SAIDI MOHAMEDI................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**TUMAINI AFWILILE MWAYOLE.............MJIBU MAOMBI**

### WITO/KUITWA SHAURINI

**KWA: TUMAINI AFWILILE MWAYOLE WA TUNDURU – MJINI**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe **20 Mwezi Machi, Mwaka 2023** saa mbili na nusu mbele ya Mheshimiwa I. J. AYO Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 19 Mwezi Januari Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TUNDURU.

---

## KUPOTELEWA NA CHETI



**OREST KAZIMOTO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S159/021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **UJIJI SEMINARY** mwaka 1990. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KIGC/RB/6203/016.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PASCHAL TEMAUNGA MNYIFUNA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T 864 BYQ**, CHASSIS NAMBA: **JT711SR4000182437** na ENGINE NAMBA: **3SFE87875454.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/78854/202**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA HANDENI LILIPO HANDENI**

**MADAI YA GHARAMA NA. 01 MWAKA 2023**

**RAJABU SENDEU................................................MSHINDA TUZO**

**DHIDI YA**

**TAMASHA MOHAMEDI.............................MSHINDWA TUNZO NA.1**
**HASSANI MOHAMEDI...............................MSHINDWA TUZO NA.2**

Hassani Mohamedi popote ulipo Rajabu Sendeu amefungua shauri mbele ya baraza la ardhi na nyumba wilaya ya handeni dhidi yako lenye namba 01/2023. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 13/03/2023 saa 3.00 asubuhi.

Hivyo basi unatakiwa kufika baraza siku hiyo na kuleta pingamizi au utetezi wako.vielezo vyote vya kesi vinapatikana katika masjala ya wazi ya baraza la ardhi nanyumba wilaya ya handeni.
Endapo hautatekeleza amri hapo juu. Shauri hili litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na uamuzi kutolewa.

Ofisi za baraza zipo wazi karibu na jingo la mkuu wa wilaya handeni. (BOMANI)

AMRI hii imetolewa na kutiwa Saini na mhuri/lakiri ya baraza hili leo tarehe 23/02/2023.

K. C. NGONYANI
MWENYEKITI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No.14 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late of the late**
**ESTER DOTTO MSAMBAZI**
**Of Kikuyu within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by RICHARD MADEJE and JOHN MBEYELA.**

### GENERAL CITATION

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the
**30th Day of MARCH, 2023**
Dated at Dodoma this 28TH day of FEBRUARY, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 60 YA MWAKA 2023**

**SALIMA YUSUFU KABAKAKI ............................MDAI**

**VERSUS**

**AMOSI CHILUNGA .......................................MDAIWA 1**

**MGUNDOI MUNDO ..................................... MDAIWA 2**

**KWA: MGUNDOI MUNDO**

**POPOTE ULIPO.**


**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 07.03. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 13 ya mwezi wa FEBRUARI, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**SHABAN IDDI SHABANI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S.1247/0221** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. MARK'S SEKONDARY** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/78376/2023.**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**VERONICA PATRICK MCHELE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S0454/0538** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NGARENARO SEKONDARI** mwaka 1999. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/78627/2023.**

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042,**
**Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ZIARA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NAPE NNAUYE KATIKA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akisoma gazeti la The Guardian alipotembelea vyombo vya habari vya IPP Mikocheni, Dar es Salaam jana. Wengine ni Mhariri Mtendaji wa gazeti hilo, Wallace Mauggo (kulia), Mkurugenzi wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Joyce Luhanga (wa pili kushoto), Kaimu Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Epson Luhwago (wa nne kulia) na viongozi wengine. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**




Waziri Nape Nnauye (wa nne kushoto), akiwa pamoja viongozi mbalimbali wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL). Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga (wa tatu kushoto), Kaimu Meneja Mkuu, Srinivas Chintaluri (wa nne kulia), Kaimu Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Epson Luhwago (wa pili kushoto), Meneja Uzalishaji, Balasubramaniyan Venkadachalam (kulia), Mhariri Mtendaji wa The Guardian, Wallace Mauggo (wa pili kulia), Meneja wa Fedha, Samweli Orgeness na Mkurugenzi wa Biashara, Ajay Goyal.



Waziri Nape Nnauye, akipata maelezo kuhusu uchapishaji wa magazeti kutoka kwa Meneja Uzalishaji wa TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (wa pili kulia).



Waziri Nape Nnauye akihojiwa na mtangazaji wa kipindi cha michezo cha Kipenga, Said Msumi, alipotembelea studio za East Africa Radio.



Waziri Nape Nnauye akimsikiliza Mkurugenzi wa Radio One, Deogratius Rweyunga, alipotembelea studio za redio hiyo.



Waziri Nape Nnauye akizungumza na waandishi wa habari wa vyombo vya IPP baada ya kumaliza ziara. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa East Africa Radio/Televisheni, Regina Mengi (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Redio One, Joyce Mhavile (kushoto) na Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga.

HABARI MICHEZO

# DODOMA JIJI SASA YATAJA KINACHOITAFUNA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji ambayo inashika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 24, na kuwa moja ya timu zinazopigana kufa kupona kusalia ligi hiyo, imesema tatizo ni wachezaji wake kutotumia nafasi nyingi wanazozipata kuweka mpira nyavuni.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo Hassan Liogope, amekiri kuwa timu iko kwenye hali mbaya kimsimamo baada ya kupoteza mechi iliyopita dhidi ya Ihefu, lakini kwa sasa wapo kwenye mazoezi wakirekebisha hali hiyo ambapo anaamini wakifanya hilo kwa kushirikiana na uongozi pamoja na wachezaji watasalia Ligi Kuu.

"Kweli hatupo kwenye nafasi nzuri na hasa baada ya kupoteza mechi iliyopita dhidi ya Ihefu, tatizo letu kubwa ni kutomalizia nafasi tunazozipata, tumelifanyia kazi hilo na tunaendelea kulifanyia kazi kwa ajili ya kulitilia mkazo mechi zetu zilizobaki.

"Mechi ijayo tunakwenda kucheza na Polisi Tanzania, itakuwa ngumu kwa sababu nayo imetoka kupoteza dhidi ya Mbeya City, tunajua kucheza na timu ambazo zipo chini si rahisi, lakini sisi tunafahamu jinsi gani ya kucheza nazo, hata sisi kwenye mzunguko wa kwanza tulikaa sana huko chini," alisema Liogope.

Hilo limeungwa mkono na mchezaji Mbwana Hamisi 'Kibacha' ambaye amesema anaamini wao kama wachezaji wakipambana, Dodoma Jiji itabaki Ligi Kuu.

"Naamini kama wachezaji tukipambana tutabaki, kwa sababu hata kwenye mechi tunazopoteza tunacheza vizuri na nafasi nyingi zinapatikana, kinachokosekana kwetu wakati mwingine ni bahati tu," alisema.

Huu ni msimu wa tatu kwa Dodoma Jiji kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini imekuwa kwenye hali mbaya, ikicheza mechi 24, kushinda saba, sare tatu na kupoteza 14, ikisalia na michezo sita tu ili kujua hatima yake ya kubaki, kushuka au kwenda kucheza mechi za mchujo.

## TANO ZA MAMA...




Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa (kushoto), akikabidhidi Sh. milioni tano kwa rais wa Yanga, Injinia Hersi Said, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa ya kununua kila goli timu hiyo itakayofunga kwenye Kombe la Shirikisho Afrika. Jumapili iliyopita Yanga ilitoka sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Real Bamako ya Mali. **MPIGAPICHA WETU**

# Geita Gold FC hesabu FA Cup

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Geita Gold FC, Mathias Wandiba, amesema nguvu na akili zao wanazielekeza katika mchezo wa hatua ya 16 bora wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup dhidi ya Green Warriors Ijumaa wiki hii.

Mechi hiyo itapigwa uwanja wao wa nyumbani wa Nyakumbo, uliopo mkoani humo, wakiwakaribisha 'Wajeda' hao wa Ligi ya Championships, ambao maskani yao ni Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Wandiba alisema wamerejea nyumbani wakitokea Ruangwa baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 ugenini katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC.

Alisema wanaendelea na maandalizi kwa kufanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na kujiimarisha kwa mchezo ujao wa Kombe la Shirikisho la Azam.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kwani ni mchezo uko kwenye ratiba kama ilivyo mechi zingine za ligi na wachezaji watakaokosekana kwa sasa hadi tupate ripoti ya daktari wa timu," alisema Wandiba.

Alisema hawana mpango wa kufanya mabadiliko ya kikosi katika mchezo huo na kwamba hilo linaweza kutokea endapo tu watapata ripoti ya daktari wa timu hiyo itakayokutana na kugundulika watawakosa baadhi ya wachezaji kwa sababu ya majeraha.

# Jang'ombe yatafuta pointi 21 kubaki Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Taifa Jang'ombe imesema inahitaji kushinda michezo saba iliyobaki ili angalau kujipa matumaini ya kubaki Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

Taifa Jang'ombe inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 10 huku ikiwa imebakisha michezo saba pekee kabla ya msimu huu kumalizika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa tiku hiyo, Omar Khamis 'Matu', alisema bado hajakata tamaa kuhusu kuiibakisha timu hiyo Ligi Kuu licha ya kwamba mashabiki wengi wa soka la Zanzibar wanawahesabu kama tayari wameshuka daraja.

Alisema matumaini yake makubwa ni kuhakikisha anapata alama 21 katika michezo saba iliyobaki ili kupata nafasi ya kuinusuru timu hiyo kushuka daraja huku akiwaombea wapinzani wake ambao wapo katika nafasi ya hatari katika msimamo wa ligi hiyo wapoteze michezo yao.

Alisema anajua katika michezo saba iliyobaki ni migumu kwa kuwa timu zote zilizo katika mstari hatari wa kushuka daraja zinapiga mahesabu kama wanayopiga ya kushinda katika michezo yao ya mwisho.

"Mchezo wetu wa 23 ndio utakaotupa mwanga, aidha tunabaki Ligi Kuu au tunashuka daraja, lakini itategemea na matokeo ya timu tatu ambazo zipo katika mstari hatari wa kushuka, tupo katika nafasi mbaya sana maana hata hiyo michezo saba iwapo tutashinda basi itategemea na matokeo yaliyopatikana kwa timu ambazo tupo nazo chini," alisema.

Hata hivyo, alisema licha ya mashabiki kupoteza matumaini kwa timu yao kubaki Ligi Kuu Zanzibar, lakini bado wananafasi kubwa ya kuifuatilia timu yao katika michezo yote iliyobaki.

Taifa Jang'ombe itashuka tena dimbani Jumamosi wiki hii kupepetana na vinara wa ligi hiyo, KMKM.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**ABRAHAM KUREJESHWA CHELSEA**
CHELSEA wanafikiria kumrejesha Tammy Abraham katika klabu hiyo kutoka AS Roma msimu huu wa majira ya joto kwani mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 25, atakuwa chaguo rahisi kuliko mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, 24. ***(Football Insider)***

**LUKAKU KURUDI DARAJANI**
MTENDAJI Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, amesema mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, atarejea Chelsea mwishoni mwa msimu wake wa mkopo wa muda mrefu, huku klabu hiyo ya Italia ikiwa bado haijaamua kama wanataka kufanya mazungumzo ya kumnunua moja kwa moja mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Sky Sports Italia)***

**STERLING ATAKIWA ARSENAL**
ARSENAL itamsajili mshambuliaji wa Chelsea, Raheem Sterling, ikiwa mshambuliaji huyo wa England atapatikana msimu wa majira ya joto, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, hataki kuondoka 'The Blues'. ***(90 Min)***

**RICE KUSHAWISHIWA UNITED**
MANCHESTER United inaamini kuwa inaweza kumshawishi Declan Rice wa West Ham kujiunga nao msimu wa majira ya joto, licha ya kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 24, kutaka kusalia London. ***(Football Insider)***

**SALAH HAONDOKI LIVERPOOL**
WAKALA wa mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, amepuuzilia mbali uvumi kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri mwenye umri wa miaka 30, anaweza kuwahama 'Wekundu' hao msimu wa majira ya joto ikiwa hawatafuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Goal)***

**HJULMAND AFUATILIWA LEICESTER**
WASAKA vipaji wa Leicester City wanafuatilia hali ya kiungo wa kati wa Lecce raia wa Denmark, Morten Hjulmand, mwenye umri wa miaka 23, baada ya Southampton kutoa ofa ya euro milioni 11 iliyokataliwa Januari mwaka jana. ***(Nicolo Schira)***

**ALVAREZ KUFUNGWA CITY**
KLABU ya Manchester City imewasilisha ombi la kuongeza mkataba wa mshambuliaji wa Argentina, Julian Alvarez mwenye umri wa miaka 23, hadi mwaka 2028. ***(Fabrizio Romano)***

**BARCA YAMTAKA ALVAREZ**
BARCELONA ni moja ya klabu zinazotathmini kama Julian Alvarez atakuwa tayari kuondoka Manchester City kwa mkopo msimu wa majira ya joto. ***(Mundo Deportivo)***

**LIVERPOOL YAMFUATILIA KANTE**
LIVERPOOL inafuatilia kwa karibu mazungumzo ya Chelsea na kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante, mwenye umri wa miaka 31, kuhusu kuongeza mkataba wake wa sasa, ambao unaisha msimu wa majira ya joto unaokuja. (***Football Insider***)

**MBAPPE MWAKA MMOJA**
KLABU ya Paris St-Germain inajaribu kumshawishi, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 24, kuongeza mkataba wake kwa mwaka mwingine hadi 2025. ***(L'Equipe, via Sport)***.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AWASHUKURU WACHEZAJI TUZO YA MCHEZAJI BORA WA FIFA

## Martinez naye ang'ara huku Scaloni akimshinda Guardiola na kutangazwa kocha bora...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Argentina na Paris St-Germain, Lionel Messi, amewashukuru wachezaji wenzake kwa mwaka wa "ndoto yake kutimia" baada ya kuchaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa wanaume kwenye Tuzo za Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa 2022.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, aliwashinda washambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe na Karim Benzema.

Messi alikuwa nahodha wa Argentina na ambayo ilitwaa ubingwa wa Kombe la Dunia nchini Qatar, na alifunga mabao 27 katika michezo 49 kwa klabu na nchi yake kwa msimu wa 2021-22.

Messi, ambaye alishinda tuzo hiyo kwa mara ya pili, alisema: "Inashangaza. Umekuwa mwaka mzuri sana na ni heshima kwangu kuwa hapa na kushinda tuzo hii," alisema.

"Bila wachezaji wenzangu nisingekuwa hapa. Nilifanikisha ndoto niliyokuwa nikitarajia kwa muda mrefu. Watu wachache sana wanaweza kufikia hilo na nimekuwa na bahati kufanya hivyo."

Katika sherehe hizo mjini Paris, Kocha Lionel Scaloni, ambaye aliongoza Argentina kutwaa taji lao la tatu la Kombe la Dunia, alitawazwa kuwa kocha bora wa mwaka wa wanaume.

Scaloni aliwashinda Pep Guardiola ambaye aliiongoza Manchester City kunyakua taji la sita la Ligi Kuu England na kocha wa Real Madrid aliyeshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, Carlo Ancelotti.

Mlinda mlango wa Aston Villa na Argentina, Emiliano Martinez, alitambuliwa kuwa kipa bora wa wanaume.

Martinez mwenye umri wa miaka 30, aliisaidia nchi yake kushinda Kombe la Dunia, akiokoa penalti nne ikiwa ni pamoja na ushindi wa mikwaju ya penalti dhidi ya Ufaransa kwenye fainali.

Kocha wa England, Sarina Wiegman, alitawazwa kuwa kocha bora wa mwaka wa wanawake baada ya kukiongoza kikosi cha England kutwaa ubingwa wa Ulaya katika ardhi ya nyumbani mwaka jana, likiwa ni taji la kwanza kuu kwa timu hiyo.

Mary Earps, anayechezea Manchester United katika Ligi Kuu ya Wanawake England, alianza mechi zote sita za England kwenye Euro 2022 huku wakishinda michuano hiyo.

Alexia Putellas wa Barcelona alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa wanawake, huku Earps akishinda tuzo ya golikipa bora wa wanawake.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,083,8
MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13


KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA: MAN UNITED SASA WANARUDI KWENYE UBORA WAO



**MANCHESTER, England**

KAMA Manchester United bado hawajarejea tayari kwenye ubora wao, watafanya hivyo "haraka au baadaye", kwa mujibu wa Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

United iliishinda Newcastle United mabao 2-0 katika fainali ya Kombe la EFL Jumapili na kushinda taji lao la kwanza katika kipindi cha miaka sita.

Ushindi huo walioupata pale Wembley, ulileta zawadi kubwa kwa msimu wa kwanza wa kuvutia chini ya Erik ten Hag, ambaye timu yake ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na bado kwenye Ligi ya Europa na Kombe la FA.

United walikuwa kwenye wakati mgumu tangu kuondoka kwa Alex Ferguson, lakini Guardiola, alipoulizwa kama sasa "wamerudi", alijibu hivi: "Kwanza kabisa, pongezi kwa United kwa Kombe la Carabao, mchezo ulikuwa wa burudani."

"Ndiyo, mapema au baadaye, inapaswa kutokea, sivyo? Haikuweza? Inapaswa kutokea. Karibu."

Akitathmini kikosi cha Ten Hag, Guardiola aliongeza: "Ni kawaida, wako katika nafasi ambayo kawaida wanapaswa kuwa.

"Lakini ukweli, kwa timu hizo, haswa Liverpool na Manchester United, katika miaka ya hivi karibuni tulichofanya ni cha kushangaza. Siku zote nilipotua hapa, nilifikiri United siku zote wangekuwapo kwa ajili ya historia, kwa kila kitu.

"Kwa hiyo, Erik anafanya kazi nzuri sana. Wachezaji, unaona jinsi wanavyojituma, jinsi wote kwa pamoja wanajaribu kufanya.

"Unapokuwa na miaka mingi, mitano, sita bila kushinda taji moja, unapokuwa na changamoto hiyo...nakumbuka tuliposhinda Kombe la kwanza la Carabao, tuliposafiri kushinda Kombe la Carabao na kila mtu alifurahi sana."

# Lewandowski kuikosa Real Madrid


**BARCELONA,**

ROBERT Lewandowski atakosa mechi ya nusu fainali ya kwanza ya Copa de Rey ya Barcelona dhidi ya Real Madrid Alhamisi kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Barca Jumatatu ilifichua kuwa Lewandowski amepata mkazo wa msuli wa paja lake la kushoto.

Viongozi hao wa LaLiga walisema mshambuliaji huyo mahiri "hayupo na kupona kwake kutaamua kupatikana kwake" siku tatu kabla ya mchuano mwingine wa Clasico kule Santiago Bernabeu.

Jeraha la Lewandowski ni pigo lingine kwa Xavi baada ya kufungwa bao 1-0 na Almeria Jumapili.



Hicho kilikuwa ni kipigo cha pili tu cha LaLiga msimu huu kwa wababe hao wa Katalunya, ambao wapo mbele ya Madrid kwa pointi saba kileleni.

Barca pia walipata pigo la kutupwa nje ya Ligi ya Europa na Manchester United wiki iliyopita na kupoteza mchezo wa marudiano pale Old Trafford kwa mabao 2-1 baada ya Lewandowski kufunga bao la 25 msimu huu.

Kikosi cha Xavi kitamenyana na 'Los Blancos' pale Camp Nou kwenye LaLiga Machi 19, mwaka huu, baada ya kumenyana na Valencia na Athletic Bilbao. Mechi ya pili ya nusu fainali ya Copa itafanyika Aprili 5, mwaka huu.

326,057/-

# MTIBWA YAKIRI MAJI MAREFU SINGIDA BS, YAIONYA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufungwa mabao 2-0 juzi kwenye Uwanja wa Liti, Singida, dhidi ya Singida Big Stars, Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma (pichani), amesema wamepoteza mechi hiyo kihalali kwa sababu wamezidiwa mbinu na wapinzani wao, lakini akaionya Simba kuwa hawatopata tena bahati kama hiyo watakapokutana nao Februari 11, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Awadh, ambaye alishawahi kuichezea Simba, alisema wamefungwa dhidi ya Singida Big Stars kwa makosa ya timu nzima na si ya mchezaji mmoja mmoja, hivyo wana kazi ya kwenda kurekebisha kabla ya mechi zao mbili zinazofuata dhidi ya KMC, Kombe la FA na Simba, mechi ya Ligi Kuu.

“Mimi nafikiri tumejitahidi sana, lakini mechi hii haikuwa ya kwetu, niwapongeze Singida, nafikiri magoli tuliyofungwa yalikuwa ni ya timu na wala si ya mchezaji mmoja mmoja, tumefanya makosa yametuhukumu, mwisho wa siku tumepoteza pointi tatu, bahati nzuri ni kwamba ligi ni kama marathon, mbio bado zinaendelea, tukitoka hapa tunakwenda kucheza na KMC tarehe nne, halafu tarehe 11 tunacheza dhidi ya Simba mechi ya Ligi Kuu, haya makosa hayatofanyika tena,” alisema kocha msaidizi huyo na kuongeza kuwa timu hizo ambazo wanakwenda kucheza nazo zisidhani zitapata mteremko kama ambao Singida Big Stars wameupata.



Kocha Mkuu wa washindi, Hans Van Pluijm, aliwasifu wachezaji wake kwa kutumia vizuri nafasi walizozipata, kwani walikuwa na tatizo la kushindwa kuweka mipira ndani ya wavu, ingawa ilikuwa ni mechi waliostahili kufunga mabao mengi.

“Mzunguko wa pili kila timu inajikakamua ili kupata pointi kwa ajili ya kutaka kupata pointi za uhakika na kusalia, zingine kukimbia janga la kushuka daraja na hata kusaka nafasi nne za juu. Na kwa sasa kila timu ikicheza na Singida Big Stars ni lazima ijitutumue, leo nimefurahi tumefunga mabao mawili, lakini tungeweza kufunga mabao mengi zaidi, mpinzani alikuwa akijaribu kucheza zaidi mipira mirefu, lakini sisi tuna wachezaji wazoefu sana kama Meddie Kagere na wenzake,” alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga na Azam FC.

Matokeo hayo yanaifanya Singida Big Stars kuwa kwenye nafasi ya nne kwa pointi 47, sawa na Azam FC iliyopo nafasi ya tatu, lakini yenyewe iko chini kwa kufunga mabao 28 dhidi ya 39 ya ‘Wanalambalamba’ hao.

Timu hizo mbili zikiwa sasa kwenye vita kali ya kuwania nafasi ya tatu ambayo moja kwa moja ina uwakilishi wa michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho barani Afrika, huku ya nne ikitegemea na timu gani itakayotwaa Kombe la FA, ambapo likitwaliwa na timu ambayo haina uwakilishi wowote kwa kutoshika nafasi tatu za juu kwenye Ligi Kuu, haina maana yoyote.

# YANGA YASHUSHA PONGEZI SIMBA

INATOKA UK. 24

Aidha, Kikosi cha Yanga ambacho kiliwasili nchini jana mchana kikitokea Mali kupitia Ethiopita, na kukabidhiwa kitita chao cha Sh. milioni tano kilichoahidiwa na Rais Samia, kimesema sasa malengo yao ni kucheza robo fainali ya michuano hiyo msimu huu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema pamoja na sare waliyoipata, haijawafanya kukata tamaa kwani kimahesabu timu yao ina nafasi kubwa ya kusonga mbele kwenye Kundi D la michuano hiyo.

“Tunamshukuru Mungu tuliondoka Dar es Salaam salama na leo kwa mapenzi yake Mwenyezi Mungu tumerejea nyumbani salama. Tumetoka Dar tukiwa na pointi tatu, tunarudi tukiwa na pointi nne kwenye kundi letu, maana yake kama klabu tumefanikiwa kuvuna pointi moja ugenini kwa hiyo hesabu zetu kwenye kundi letu bado zipo vizuri, niwaambie tu Yanga malengo yake ya kwanza makubwa mwaka huu ni kucheza robo fainali ya Kombe la Shirikisho na kwa jinsi hesabu zilivyo kila kitu kipo sawa,” alisema Kamwe.

Naye Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, kwa niaba ya Rais Samia, aliipongeza Yanga, huku akizitaka timu za Tanzania kuendelea kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa na ahadi iko palepale.

“Kwanza kabisa kwa niaba ya Rais wa Jamhuri wa Muugano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, napenda kuwapongeza Yanga kwa ushindi mlioupata kwenye mechi dhidi ya TP Mazembe wa mabao 3-1, lakini niwapongeze kwa sare ya bao 1-1 ugenini nchini Mali dhidi ya Real Bamako.

“Timu mliyocheza nayo si ndogo na wala si ya kubeza, lakini kama mmeweza kupata sare nyumbani kwao, nadhani hapa kwa Mpaka hawatoki, tunawapongeza sana na tunawatakia kila la kheri kwenye mechi yenu ya tarehe nane, najua mnacheza tena na Real Bamako hapa nyumbani Uwanja wa Benjamin Mkapa, nawapongeza sana, rais Injinia Hersi Said hongera sana.

“Hapa nimekuja na ule mzigo, mheshimiwa Rais Samia amenituma nije niwasilishe ahadi yake aliyoitoa ya kutoa Sh. milioni tano kwa kila goli ambalo Yanga watalifunga kwenye michuano yao ya Kombe la Shirikisho na Simba watalifunga kwenye michuano wanayoicheza ya Ligi ya Mabingwa Afrika,” alisema msemaji huyo.

Yanga ambayo sasa inajiandaa na mechi ya Kombe la FA Ijumaa wiki hii dhidi ya Prisons, ipo kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa michuano hiyo ikiwa na pointi nne, kundi linaloongozwa na US Monastir ya Morocco, yenye pointi saba.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/03/23 | 20:30 | Southampton FC vs Leicester City | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 04/03/23 | 20:30 | Tenerife CD vs SD Eibar | 2.36 | 2.80 | 3.40 |
| 03. 04/03/23 | 20:45 | FC Volendam vs FC Emmen | 2.60 | 3.35 | 2.60 |
| 04. 04/03/23 | 22:45 | ACF Fiorentina vs AC Milan | 2.80 | 3.20 | 2.48 |
| 05. 04/03/23 | 22:45 | Standard Liege vs KVC Westerlo | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 06. 04/03/23 | 23:00 | CD Mirandes vs Real Oviedo | 2.48 | 2.90 | 3.15 |
| 07. 05/03/23 | 14:30 | Spezia Calcio vs Hellas Verona | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 08. 05/03/23 | 15:30 | Hansa Rostock vs Karlsruher SC | 2.70 | 3.30 | 2.50 |
| 09. 05/03/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Espanyol Barcelona | 2.24 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/03/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Everton FC | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 11. 05/03/23 | 19:30 | Liverpool FC vs Manchester United | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 05/03/23 | 19:30 | VfL Wolfsburg vs Eintracht Frankfurt | 2.43 | 3.40 | 2.75 |
| 13. 05/03/23 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.90 | 3.00 | 2.55 |
| 14. 05/03/23 | 21:00 | Santa Clara Azores vs Vitoria SC Guimaraes | 2.70 | 3.15 | 2.60 |
| 15. 05/03/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Go Ahead Eagles | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 16. 05/03/23 | 22:45 | AS Roma vs Juventus Turin | 2.37 | 3.05 | 3.10 |
| 17. 05/03/23 | 22:45 | Stade Rennes vs Olympique Marseille | 2.75 | 3.35 | 2.45 |

## MECHI ZA USHINDI

“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE “2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 01/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1272 | Bhayangkara Surabaya Utd vs Psis Semarang | 1.87 | 3.38 | 3.59 |
| 14:00 | 2221 | Pyunik Yerevan vs Shirak Gyumri | 1.35 | 4.15 | 8.51 |
| 14:30 | 3488 | Bsk Bijelo Brdo vs HNK Sibenik | 3.36 | 3.36 | 1.98 |
| 15:15 | 1084 | Kuala Lumpur vs Johor Darul Takzim | 8.63 | 4.93 | 1.26 |
| 16:00 | 1364 | Kedah vs Terengganu | 2.43 | 3.39 | 2.47 |
| 16:00 | 4370 | Penang vs Negeri Sembilan | 4.10 | 3.34 | 1.77 |
| 16:00 | 4572 | Saint George FC vs Dire Dawa Kenema FC | 1.36 | 4.24 | 7.87 |
| 16:00 | 4879 | FK Mladost Gat vs FK Napredak | 2.43 | 2.92 | 2.82 |
| 16:30 | 1504 | Hungry Lion vs Cape Town All Stars | 2.25 | 2.54 | 3.70 |
| 16:30 | 4018 | Minerva FC vs Churchill Brothers | 1.60 | 3.68 | 4.71 |
| 16:30 | 5962 | Baroka FC vs Ajax Cape Town | 2.62 | 2.67 | 2.83 |
| 17:00 | 2356 | Urartu vs Van Yerevan | 1.50 | 3.73 | 6.01 |
| 17:00 | 4239 | FK Trajal vs OFK Vrsac | 2.25 | 2.89 | 3.14 |
| 17:00 | 4521 | Dinamo Zagreb vs Lokomotiva Zagreb | 1.35 | 4.66 | 7.04 |
| 17:00 | 5715 | CS Mioveni vs Voluntari | 2.72 | 2.99 | 2.58 |
| 18:00 | 2534 | Spartak Subotica vs Novi Pazar | 2.44 | 3.02 | 2.71 |
| 18:30 | 4760 | Manama Club vs Riffa Club | 2.48 | 3.00 | 2.74 |
| 18:30 | 5365 | Al Hidd Club vs Sitra Club | 2.85 | 2.95 | 2.44 |
| 19:00 | 2085 | Ceske Budejovice vs Zbrojovka Brno | 2.02 | 3.52 | 3.11 |
| 19:00 | 2223 | Universitatea Craiova vs Argesul Pitesti | 1.54 | 3.68 | 5.88 |
| 19:00 | 2635 | Bahir Dar Kenema FC vs Welayta Dicha FC | 1.77 | 3.00 | 4.20 |
| 19:00 | 3862 | Farco FC vs Arab Contractors | 3.49 | 2.80 | 2.26 |
| 19:00 | 3966 | Slovacko vs Bohemians | 2.18 | 3.62 | 2.74 |
| 19:00 | 4039 | Lamia vs PAOK | 8.92 | 4.25 | 1.33 |
| 19:00 | 4121 | Macva Sabac vs FK Radnicki Sremska Mitrovica | 2.50 | 2.65 | 2.80 |
| 19:00 | 4421 | Slovan Liberec vs Sparta Prague | 2.60 | 3.59 | 2.29 |
| 19:00 | 5883 | Budafoki Mte vs Kisvarda FC | 6.01 | 4.09 | 1.45 |
| 19:30 | 3678 | KKS 1925 Kalisz vs Slask Wroclaw | 4.97 | 3.93 | 1.55 |
| 20:00 | 1356 | Dinamo Moscow vs Kryliya Sovetov | 1.77 | 3.63 | 3.84 |
| 20:00 | 1411 | NK Osijek vs Hajduk Split | 2.69 | 3.11 | 2.46 |
| 20:00 | 1750 | Mladost Lucani vs Cukaricki St | 3.24 | 3.18 | 2.05 |
| 20:00 | 3981 | Slavia Prague vs Vyskov | 1.11 | 7.23 | 17.56 |
| 20:15 | 3813 | Nantes vs Lens | 4.09 | 3.54 | 1.82 |
| 20:45 | 1820 | Toulouse vs Rodez Aveyron | 1.31 | 5.16 | 8.53 |
| 21:00 | 5913 | Olympiakos vs AEK Athens | 2.20 | 3.26 | 2.95 |
| 21:30 | 5307 | Botosani vs Rapid Bucuresti | 3.36 | 3.10 | 2.13 |
| 22:00 | 1548 | Copenhagen vs Vejle BK | 1.42 | 4.25 | 6.22 |
| 22:00 | 1763 | Heerenveen vs Feyenoord | 4.46 | 3.94 | 1.61 |
| 22:00 | 2103 | Paksi FC vs Vasas SC | 1.98 | 3.42 | 3.31 |
| 22:15 | 1169 | Southampton vs Grimsby | 1.28 | 5.26 | 8.19 |
| 22:15 | 3951 | St. Gallen vs FC Basel | 2.04 | 3.53 | 2.97 |
| 22:15 | 4739 | FC Sion vs FC Lugano | 2.66 | 3.22 | 2.36 |
| 22:30 | 3448 | Burnley vs Fleetwood Town | 1.26 | 5.27 | 8.98 |
| 22:30 | 5877 | LKP Motor Lublin vs Rakow Czestochowa | 7.88 | 4.56 | 1.33 |
| 22:45 | 2333 | Arsenal vs Everton | 1.31 | 4.82 | 8.46 |
| 22:45 | 3876 | Manchester Utd vs West Ham | 1.60 | 3.77 | 4.90 |
| 22:55 | 5081 | Sheffield Utd vs Tottenham | 4.09 | 3.56 | 1.75 |
| 23:00 | 1534 | Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.94 | 3.00 | 2.43 |
| 23:00 | 2413 | Marseille vs Annecy FC | 1.18 | 6.78 | 12.96 |
| 23:00 | 5622 | Liverpool vs Wolverhampton | 1.44 | 4.31 | 6.08 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Machi 1, 2023

Nipashe




UKURASA 22

## Guardiola: Man United sasa wanarudi

NI MESSI TENA...



Mshambuliaji wa Argentina na Paris Saint-Germain, Lionel Messi (kushoto), akipokea Tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Fifa 2022 kwa Wanaume kutoka kwa Rais wa Fifa, Gianni Infantino, kwenye sherehe za utoaji wa tuzo za shirikisho hilo zilizofanyika jijini Paris, Ufaransa usiku wa kuamkia jana. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YASHUSHA PONGEZI SIMBA SC

●●●Ni kwa ilichokifanya Uganda, yamwahidi Rais Samia Real Bamako hawatatoka kwa Mkapa na...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imewapongeza watani zao wa jadi Simba kwa kushinda mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini dhidi ya Vipers Jumamosi iliyopita, huku nayo ikiahidi kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu.

Akizungumza baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jana, Rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said, alisema ilikuwa ni wiki ambayo timu zote za Tanzania zilielekea kupata ushindi ugenini, lakini kwa bahati mbaya kwao haikuwa hivyo, na kwamba anaahidi kuwa watashinda na kupata pointi tatu kwenye mechi ya Machi 8, mwaka huu (Jumatano ijayo), itakayochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Real Bamako ya Mali.

"Kwanza napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa mzigo huu wa pesa ambao ni kama zawadi ya kuleta hamasa kwenye klabu zetu za Simba na Yanga ambazo zinashiriki michuano ya kimataifa na tunawapongeza Simba kwa ushindi wao wa ugenini, lakini tunawapongeza wachezaji wetu wa Yanga na klabu nzima kwa sare ya ugenini ambayo naweza kusema, wote tulikuwa tunaelekea kupata pointi tatu, lakini ni mipango ya Mungu haikuwezekana.

"Nawapongeza wachezaji wetu kwa sababu huko ugenini hali haikuwa nzuri sana, hali ya hewa na mazingira ya ugenini, lakini tumeonyesha ni jinsi gani tuna kikosi imara ambacho kinaweza kupata matokeo sehemu yoyote na kwa hamasa hii namuahidi mheshimiwa siku ya tarehe nane tutakaporudiana na Real Bamako, sisi tutaendelea kupata matokeo mazuri," alisema Injinia.

Jumamosi iliyopita, Simba iliichapa Vipers bao 1-0 kwenye Uwanja wa St Mary's Chitende, Entebbe nchini Uganda, na siku ya pili, Yanga ikiwa kwenye Uwanja wa 26 Mars, Bamako nchini Mali, ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Real Bamako, Kombe la Shirikisho barani Afrika.

INAENDELEA UK. 23

## Mo aanika sababu kumteua Try Again

**Na Saada Akida**

Rais wa Heshima na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, amemteua kwa mara nyingine Salim Abdallah 'Try Again', kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Wekundu wa Msimbazi hao.

Dewji amefanya uteuzi huo katika hafla fupi ya kuwaaga wajumbe waliomaliza muda wao akiwamo Kassim Dewji, Mwina Kaduguda na Hussein Kita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mohamed Dewji, alisema kuwa anaimani na Try Again' ndio maana amempa nafasi nyingine na anaamini ataendelea kuiongoza Simba kufikia mafanikio makubwa barani Afrika.

"Umefanya kazi nzuri ninaimani na wewe, nategemea utaifikisha Simba kwenye mafanikio makubwa ya soka barani Afrika na duniani kwa ujumla, " alisema Mo Dewji.



Kwa upande wa Try Again, alisema anafurahi kuwa sehemu ya uongozi katika bodi hiyo na kwamba atahakikisha anaendelea kuitendea haki nafasi aliyopewa kwa mara nyingine kuifanya Simba kuwa imara.

"Asante sana ndugu Mo Dewji kwa imani yako juu yangu, nakuahidi utendaji bora kwenye nafasi hii ili kwa pamoja tunaweza kuifikisha Simba kwenye mafanikio makubwa ambayo inastahili," alisema Try Again.

Mo Dewji alitumia hafla hiyo kuwapa vyeti wajumbe watatu ambao ni Murtaza Mangungu, Haroub Seleman na Asha Baraka ambao bado wako katika bodi hiyo wakipita kwa upande wa wanachama baada ya kuchaguliwa hivi karibuni.

Mo Dewji alimteua Try Again kuchukua nafasi yake Septemba mwaka 2021, baada ya kubanwa na shughuli zake za biashara ambapo amefanya kazi nzuri kabla ya kumteua tena kuongoza bodi hiyo.

Wakati huo huo kikosi cha Simba kimeingia kambini kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho la Azam (FA Cup) dhidi ya African Sports kutoka Tanga.

Mchezo huo utakaopigwa kesho (Alhamisi) katika Uwanja wa Uhuru saa 10:00 alasiri, awali ulitangazwa ungepigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa saa 1:00 usiku.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >